# MCHANGO WA VIJANA WA KULETA UKOMBOZI KATIKA *YASINYA, ZINGUO LA MZUKA NA* "MWAVYAJI WA ROHO"

**NA**

**WAMBUI FLORENCE NJERI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2018**

## UNGAMO

**Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.**

**Sahihi------------------------** **----------------------------------**

**Wambui Florence Njeri** **Tarehe**

**Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**Sahihi------------------------------** **--------------------------------**

**Dkt. Evans Mbuthia** **Tarehe**

**Sahihi-----------------------------** **-----------------------------------**

**Dkt Prisca Jerono** **Tarehe**

## TABARUKU

Naitabarukia kazi hii mamangu mzazi Mary Wambui na ndugu yangu Eric Karira kwa jitihada zao ili nipate elimu. Pia Mume wangu Samuel Maina na mtoto wangu Mitchelle Njeri .

# SHUKRANI

Pamoja na jitihada zangu palikuwepo na ushirikiano wa wengi walionipa nguvu na kunishika mkono kuiwezesha kazi hii kukamilika. Hivyo sina budi kuwashukuru. Namshukuru Mola kwa uhai na kuniwezesha kufanya utafiti huu hadi kuukamilisha nikiwa na afya njema**.**

Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt Evans Mbuthia na Dkt PriscaJerono kwa kuniongoza, kunielekeza na hata kwa uvumilivu wao mkubwa katika safari ya uandishi wa tasnifu hii. Mola awaneemeshe.

Ningependa kuwashukuru wahadhiri wa idara ya Kiswahili ambao waliniwezesha kutimiza ndoto yangu. Hawa ni pamoja na : Prof. Iribe, Prof. Habwe, Prof. Rayya, Prof. Kineene wa Mutiso,  Dkt. Zaja, Dkt. Mweri, Mwalimu Sanja na Mwalimu Ndung'u. Mungu awabariki na awaongeze busara kwa kazi zenu.

Kamwe siwezi kuwasahau wenzangu tuliokuwa nao katika safari hii nikianza na Lilian Nzambi, Claris Chaniro, Dominic Muinde na Raymond Owala ambao tulitembea pamoja katika kuhimizana na kushauriana ili kutimiza malengo yetu. Wengine ni Jackline, Victor, Christine, Vero, Nancy,  Rose, Muita, Ninah, Kithinji Thuranira, Msamali, Nancy, George na Okello.

Familia yangu imechangia pakubwa katika ufanisi wangu kwa hali na mali. Shukrani nyingi ni kwa mume wangu mpendwa Samuel Maina ambaye alikuwa mvumilivu katika muda huu wote wa masomo yangu ahsante kwa kumtunza mtoto wetu nilipokuwa masomoni na hata kwa ushauri ulionipa na kunitia moyo ulikuwa mhimili mkuu katika kozi hii. Namshukuru mtoto wangu Mitchell aliyenikosa wakati alinihitaji sana lakini akajikaza.  Ninamshukuru Mamangu kwa kuniwekea msingi mkuu katika masomo yangu, kwa kuniombea na kuendelea kunihimiza katika kumaliza masomo yangu. Mungu ambariki na amwongeze miaka mingi. Siwezi kumsahau ndugu yangu Eric Karira ambaye pia alinifaa katika ushauri hata kwa hali na mali Mungu akujalie. Ndugu zangu Amos, Njau, na Tom ahsanteni kwa ufaafu wenu.Namshukuru pia Baba mkwe Jackson Thugu aliyekuwa mshauri mkuu katika safari hii. Mungu akujalie mema na neema zake zikutoshe.

Shukrani zingine ziwaendee mwalimu mkuu shule ya upili ya Cura Bw. Njoroge na naibu wake Bi. Njuguna ambao wamekuwa wakinipa moyo na hata kunihimiza katika kumaliza kozi hii mungu awabariki.

# IKISIRI

Katika tasnifu hii tulishughulikia mchango wa vijana katika kuleta ukombozi katika kazi za Leonard Sanja ambazo ni “Mwanyaji wa Roho” katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na hadithi Nyingine* (2011) *Zinguo la Mzuka* (2011*) na Yasinya* (2012). Tulitumia Nadharia ya Uhalisia kuchanganua kazi hizi tatu. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza nafasi ya vijana katika kuleta ukombozi katika kazi hizi tatu na pia kuonyesha changamoto ambazo vijana wanakubana nazo katika kuleta ukombozi. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ambapo mtafiti alisoma kazi zilizoteuliwa pamoja na vitabu vingine vilivyohusiana na utafiti wetu ili kupata data iliyohitajika. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti pamoja na nadharia ya uhalisia. Uchanganuzi ulifanywa kwa njia ya maelezo.Utafiti huu ulibaini kuwa vijana wamepewa nafasi kubwa ya kupigania haki za wanaodhulumiwa ili kuleta ukombozi. Ni katika kuungana kwa vijana hawa ambapo walifaulu kuleta ukombozi katika kazi hizi tatu. Hata hivyo, vijana hawa wamekumbwa na matatizo si haba katika juhudi zao za kuleta ukombozi.Licha ya changamoto hizi, utafiti wetu ulibaini kuwa wahusika vijana katika kazi hizi tatu wametoa mchango mkubwa katika juhudi za ukombozi wa jamii zao.

## YALIYOMO

UNGAMO ..... II
TABARUKU ..... III
SHUKRANI ..... IV
IKISIRI ..... VI

## SURA YA KWANZA

## YALIYOMO

1.1 Usuli wa mada ..... 1
1.2 Tatizo la Utafiti ..... 4
1.3 Maswali ya Utafiti ..... 5
1.4 Malengo ya Utafiti ..... 5
1.5Sababu za Kuchagua Mada ..... 5
1.6 Upeo na Mpaka ..... 6
1.7 Msingi wa Kinadharia ..... 6
1.7.1 Mihimili ya nadharia ya Uhalisia ..... 10
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada ..... 11
1.9 Njia za utafiti ..... 16
1.10 Hitimisho ..... 17

## SURA YA PILI

## UKOMBOZI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

2.0 Utangulizi ..... 18
2.1 Afrika ya Kale ..... 19
2.2 Kipindi cha ukoloni ..... 20
2.3 Baada ya Uhuru ..... 23
2.3.1 Ukoloni Mamboleo ..... 24
2.3.2 Uongozi Mbaya ..... 25
2.3.2.1 Ufisadi ..... 26
2.3.2.2 Utabaka ..... 29
2.3.2.3 Ukosefu wa haki ..... 30
2.3.2.4 Umasikini ..... 31
2.3.3 Hitimisho ..... 32

**SURA YA TATU**

**MCHANGO WA VIJANA WA KULETA UKOMBOZI KATIKA KAZI ZA LEONARD SANJA**

3.1 Utangulizi ....... 33
3.1.1 Muhtasari Wa "Mwavyaji wa Roho" ....... 33
3.1.2 Muhtasari wa Zinguo La Mzuka ....... 34
3.1.3 Muhtasari wa Riwaya ya Yasinya ....... 35
3.2.1 Ukombozi dhidi ya umaskini ....... 39
3.2.2 Dhuluma kwa wanawake ....... 43
3.2.3 Ukombozi dhidi ya Ufisadi ....... 47
3.2.4 Ukombozi wa kimawazo ....... 51
3.2.5 Ukombozi wa kisiasa ....... 52
3.2.6 Ukoloni mamboleo ....... 55
3.2.7 Unyanyasaji wa wafanya kazi ....... 56
3.2.8 Ukombozi wa Kimaadili ....... 57
3.2.9 Uharibifu wa mazingira ....... 58
3.2.10 Dhuluma kwa wafungwa ....... 59
3.2.11 HITIMISHO ....... 60

**SURA YA NNE**

**CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA VIJANA KATIKA HARAKATI ZA KULETA UKOMBOZI**

4.1 Utangulizi ....... 62
4.2.1 Usaliti ....... 62
4.2.2 Kutowajibika kwa maafisa wa polisi ....... 64
4.2.3 Umasikini ....... 64
4.2.4. Vitisho ....... 66
4.2.5. Utepetevu katika utekelezaji wa sheria ....... 67
4.2.6 Matumizi Mabaya ya Mamlaka ....... 68
4.2.7 Dhuluma dhidi ya vijana ....... 68
4.2.8 Ukosefu wa Haki Mahakamani ....... 70
4.3 Hitimisho ....... 70

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi ..... 72
5.2 Muhtasari wa Matokeo ..... 72
5.3 Hitimisho ..... 73
5.4 Mapendekezo ..... 74
MAREJELEO ..... 75

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli wa mada

Utafiti wetu ulichunguza suala la vijana na ukombozi katika kazi za Leonard Sanja ambazo ni: riwaya *Yasinya* (2014), tamthilia *Zinguo la Mzuka* (2011) na "Mwavyaji wa Roho" katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na hadithi nyingine* (2011). Katika kazi hizi, tulinuia kutalii jinsi vijana wanahusika na suala la ukombozi.Tulitumia nadharia ya uhalisia katika uchanganuzi wa kazi hizi tatu.

Uhalisia huelezwa kama uwasilishaji wa masuala kuhusu jamii kama yalivyo katika uhalisia wake. Utafiti wetu ulichukulia uhalisia kwa misingi ya uwasilishaji wa matukio kama yanavyoonekana katika jamii na pia wahusika wanaoshahibiana na binadamu wa kawaida katika utenda kazi wao na hata mawasiliano yao.

Kulingana na Katiba ya Kenya (2010), kijana ni mtu wa jinsia ya kiume au ya kike aliye na umri wa kati ya miaka 15 na 35. Ufafanuzi huu unalenga kubainisha dhana kijana kwa misingi ya umri. Majukumuya vijana hubadilika kila uchao kulingana na mabadiliko ya jamii husika.Vijana katika maisha ya sasa wana majukumu yaliyo tofauti na wale wa jadi na kwa hivyo kazi za kifasihi zinazohusu vijana, zinawasawiri vijana katika mazingira ya kisasa. Utafiti wetu unachukulia kijana kama inavyoeleza katiba ya Kenya.

Katika kazi tulizozitafiti, wahusika vijana katika vyuo vikuu, shule za upili na pia wale ambao wanatafuta ajira, wamepewa nafasi kubwa na mwandishi wa kazi hizi. Wahusika hawa wanajitokeza katika jamii ambazo zina viongozi dhalimu hali ambayo inachangia kupigania uhuru wao na wa jamii nzima.

Dhana ya ukombozi inaweza kuelezwa kama jitihada za kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa, ili watu wawe huru kuna haja ya mapambano dhidi ya wanyanyasaji.

Ukombozi pia unaweza kuhusishwa na hali ambapo mtu binafsi anajikomboa kutoka kwa hali ya mateso au ya unyanyasaji. Yaani mtu ana uwezo wa kujikomboa kutoka kwa hali mbaya ya maisha inayomnyima haki yake au hata hali inayomdunisha.

Utafiti wetu uliangazia ukombozi kwa maana ya kuwatoa watu kutoka udhalimu na pia hali ya mtu kujinasua kutokana na hali zinazomzuia kuishi kwa njia bora. Katika utafiti wetu, tulichunguza aina mbalimbali za ukombozi kama vile: ukombozi dhidi ya umaskini, ukombozi wa kiuchumi, ukombozi wa kielimu, ukombozi wa maadili yasiyokubalika na jamii na hata ukombozi wa unyanyasaji ambao unahusishwa na jinsia ya mtu, unaoletwa na vijana katika kazi husika. Kwa hivyo kusudi letu lilikuwa kuchunguza jinsi wahusika vijana wanachangia katika suala nzima la ukombozi dhidi ya maonevu mbalimbali katika kazi tulizoteua.

Baada ya kuungana kwa waafrika katika mataifa mbalimbali bila ya kujali mipaka ya kikabila, kinasaba wala kitabaka, walitimiza ari yao ya kuupigania uhuru wao waliokuwa wamenyimwa na wakoloni. Msukumo huu ulisababishwa na dhuluma walizofanyiwa waafrika na vile vile hali ya kuwa na kiu cha kutaka kujikomboa ili wawe na uhuru wa kujitawala.

Kufikia miaka ya sabini, mengi ya mataifa katika bara ya Afrika yalikuwa yamejikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni.Hatamu ya uongozi ilichukuliwa na baadhi ya waafrika wa umri wa makamu waliokuwa wamepigania uhuru. Viongozi hawa walichukuliwa kama ndugu na pia waliaminiwa kuwa wenye hekima, uzoefu wa maisha na zaidi ya hayo walikuwa wamekomaa kisiasa. Kwa hivyo, walitarajiwa kuwaongoza ndugu zao kwa usawa kila mwananchi akifurahia matunda ya ukombozi.

Baada ya waafrika kujinyakulia uhuru matumaini yao yalikosa kutimia. Viongozi wa kiafrika badala ya kudhihirisha kuwa ukombozi dhidi ya mkoloni mkongwe ulikuwa na mazao bora, wao waliendeleza ufisadi, ubinafsi, ukatili na dhuluma nyinginezo walizokuwa wamerithi kutoka kwa wakoloni wa kimagharibi.

Takribani miaka hamsini hivi tangu nchi za kiafrika zilipojinyakulia ‘ uhuru’ viongozi wa Kiafrika wamekuwa wakiendeleza dhuluma mithili ya wakoloni wa hapo awali. Dhuluma hizi zimekuwa kichocheo kwa wananchi na vijana kuendelea kupigania haki zao.

Baada ya miongo kadhaa ya utawala wa waafrika vijana walilazimika kupigania uhuru wa pili dhidi ya mwafrika dhalimu ambaye amefuata njia za mkoloni wa kimagharibi za kujilimbikizia mali bila ya kumuwazia mwananchi mwenzake.

Wahusika vijana wanakumbwa na changamoto anuwai kama vile ufuska, ufisadi unaoendelezwa na viongozi dhalimu, unyakuaji wa mashamba, pamoja na maovu mengine ya kimaadili. Viongozi dhalimu ambao wako mamlakani wanatumia uongozi kujinufaisha na kuwasahau vijana na wananchi waliowachagua. Baadhi ya viongozi ndio wanaendeleza biashara haramu za uuzaji wa madawa ya kulevya pamoja na kujinyakulia mashamba huku wanajamii wengine wakiendelea kutaabika kwa kukosa makao.Ufisadi unaoendelezwa na viongozi dhalimu unaziathiri nchi zao hivi kwamba hata huduma za matibabu ni chache na pia si za kuridhisha.

Ukosefu wa ajira pia ni jambo ambalo linasababisha vijana kujiingiza katika maovu ilimradi wajikimu kimaisha .Vijana waadilifu ni viungo muhimu sana katika ujenzi wa jamii katika siku zijazo na pia ni tegemeo katika maendeleo ya nchi ikikumbukwa hawa ndio wana nguvu za kufanya kazi baada ya masomo. Katika kazi tulizoshughulikia vijana walishuhudiwa wakiungana bila ya kujali tofauti zao za kikabila au kijinsia katika shughuli zao za kila siku kwa mfano katika kutetea haki zao.Ni kutokana na haya ambapo kuna haja ya kuangazia majukumu yao katika jamii kwa kuwa wao ndio tegemeo la siku zijazo za usoni na kwa hivyo jamii inapowasahau vijana ni sawa na kusahau kuna kesho.

Kama tulivyoeleza hapo awali, kazi za kifasihi huiangazia jamii kama ilivyo.Utafiti huu uliwaangazia vijana na hivyo kubainisha uwezo walionao vijana katika kuleta ukombozi wa jamii nzima dhidi ya changamoto zinazoikumba jamii kwa kuwa ulichunguza nafasi muhimuya vijana katika kuleta ukombozi wa jamii mpya isiyo na utengano na inayozingatia haki za wote.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulijishughulisha kubainisha na kuchanganua suala la vijana na ukombozi katika kazi tatu za Leornard Sanja ambazo ni: *Yasinya* (2014), *Zinguo la Mzuka* (2011) na hadithi ya Mwavyaji wa Roho katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na hadithi nyingine (2011).*

Kulingana na sensa ya mwaka wa 2009, vijana wamebainika kuwa ndio na idadi kubwa sana hapa nchini Kenya. Utafiti huu ulichochewa na vijana katika kazi hizi za mwandishi . Tulibaini kwamba kazi hizi zina wahusika vijana na wanaopewa majukumu mbalimbali yanayowaelekeza katika mchakato wa ukombozi wa jamii katika fasihi husika. Mwandishi wa kazi hizi amewapa vijana nafasi iliyo muhimu katika ujenzi wa jamii huru.Kazi hizi pia ni kielelezo cha hali halisi ya vijana katika jamii halisia.

Jamii katika kazi hizi zilizoteuliwa zinakumbwa na dhuluma nyingi zinazotokana na uongozi dhalimu licha ya kuwa walikuwa wamejinyakulia uhuru. Utafiti huu ulichochewa kuchunguza na kufafanua juhudi za vijana katika kupigania ukombozi na changamoto wanazokutana nazo. Hali kadhalika kubainisha vichochezi vinavyowasukuma vijana katika mchakato huu mzima.

Utafiti huu ulichunguza nafasi ya vijana ya kuleta ukombozi kwa kuwa vijana kama viungo muhimu katika jamii wanahitaji kuangaziwa kutokana na majukumu ambayo wanatarajiwa kutekeleza. Wingi wa vijana una athari kubwa sana katika jamii ikiwa ni pamoja na uamuzi wa viongozi katika upigaji wa kura. Ukombozi wa vijana si wa kisiasa tu bali unyanyasaji mwingine kama vile wa kiuchumi, ukosefu wa elimu na hata kutengwa kijinsia.

Utafiti wetu ulinuia kuchunguza jinsi vijana wanakabiliana na suala la ukombozi wa aina mbalimbali ili kuonyesha jinsi jamii inavyoweza kuwategemea vijana katika kuleta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayoikabili na pia changamoto zinazowakumba katika kutekeleza azma yao.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unajibu maswali yafuatayo:

(i) Vijana wanaleta ukombozi wa aina gani katika kazi husika?

(ii) Je ni vichochezi vipi vinawasukuma vijana kupigania ukombozi?

(iii)Ni matatizo yapi yanawakumba vijana katika kuleta ukombozi ?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

(i) Kuchunguza aina za ukombozi zinazoletwa na vijana katika kazi zilizoteuliwa

(ii) Kuangazia vichochezi vya kupigania ukombozi katika kazi zilizoteuliwa za Leonard Sanja.

(iii) Kubainisha changamoto zinazowakumba vijana katika kuleta ukombozi katika kazi husika.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Japo imebainika kuwa vijana ndio wenye idadi kubwa sana hapa nchini Kenya na vilevile asilimia kubwa yao wameelimika, wengi wanaishi maisha ya uchochole kutokana na ukosefu wa ajira. Tatizo hili limechangia matatizo wanayopitia vijana hapa nchini katika harakati zao za kujaribu kujikimu kimaisha na kwa hivyo kujiingiza katika madawa ya kulevya, uhalifu na hata maovu mengine yanayopatikana katika jamii.Viongozi pamoja na wanaomiliki asasi za uzalishaji mali, wanachukua nafasi hii hasi ya vijana kuwatumia kisiasa na hata kuwahusisha na uhalifu mwingine.Kwa hivyo utafiti huu ulinuia kuchunguza jinsi mwandishi alivyowasawiri vijana na pia nafasi yao katika kuisaidia jamii kujinasua kutokana na matatizo yake.

Tuliamua kuangazia kazi zake tatu katika tanzu tatu tofauti ili tupate picha kamili ya mwandishi huyu kuhusiana na vijana Ingawaje inafahamika kuwa kila utanzu, una sifa zake bayana zinazomfanya mwandishi kuandika kwa njia mahsusi tulidhamiria kuzichunguza zote ili tupate msimamo wake katika hali hizi zote.

## 1.6 Upeo na Mpaka

Utafiti wetu ulijikita katika kuchanganua suala la vijana na ukombozi katika kazi tatu ambazo ni, *Yasinya* (2014), *Zinguo la Mzuka* (2011) na hadithi fupi "Mwavyaji wa Roho" katika *Mwavyaji wa Roho na hadithi nyingine* (2011). Utafiti wetu ulijikita tu kwenye kazi hizi tatu ili kubainisha mchango wa vijana katika kuleta ukombozi. Tuliongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo inasisitiza usawiri wa hali ya maisha kama yalivyo katika uhalisia wake. Tulijikita katika wahusika vijana ili kuchunguza mchango wao katika kuleta ukombozi wa ukosefu wa elimu, hali duni ya kiuchumi,uozo wa kimaadili na hata ukombozi unyanyasaji wa kijinsia.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uhalisia katika kuzihakiki na kuzichanganua kazi teule. Nadharia ya uhalisia ilizuka katika karne ya kumi na tisa kwa lengo la kuupinga ulimbwende. Uhalisia hujikita katika mambo yanayopatikana katika jamii na yanayoweza kuthibitika.

Donna (2007) anasema uhalisia una misingi yake katika nchi ya.Ufaransa mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Waandishi walianza kuandika kazi za kifasihi ambazo zilikuwa na sifa za kipekee kama vile, msuko sahili, wahusika waliowakilisha tabaka la kati au la chini. Wahusika hawa walikaribiana na watu halisia katika mazungumzo yao. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ya uhalisia ni Flaubert(1857).Inaakisiwa kuwa kazi hii ilikuwa ya kwanza kudhihirisha sifa za uhalisia.Kulingana naye, kazi za kifasihi zinapaswa kuangazia masuala ya jamii kama yalivyo katika hali halisi.

Donna (2007) anaendelea kueleza kuwa kazi za kifasihi zilizohusishwa na uhalisia nchini Marekani, zilitokana na kupingwa kwa ulimbwende kati ya mwaka wa 1865 hadi 1910. Karne ya kumi na tisa kulikuwepo na maendeleo mengi ya ukuaji wa viwanda. Miji ilikua kwa kiwango kikubwa kutokana na uzalishaji wa mali. Hali hii iliibua mgawanyiko kati ya mabwenyenye na wale wa tabaka la chini au wachochole. Kutokana na haya, palikuwa na haja ya kufafanua hali hii ya maisha kupitia kwa fasihi. Kwa hivyo nadharia ya uhalisia inahusishwa na kipindi ambapo palikuwepo na hali ya unyanyasaji wa tabaka la chini kutoka kwa mabwenyenye.

Nadharia hii ya uhalisia inalenga uwasilishaji wa mambo yalivyo kwa uwazi. Katika kufanya hivi wanaosoma kazi fulani wataona matukio na hali yao halisi ya maisha kama yalivyo na kwa hivyo kuwawezesha kujifikiria kulingana na hali wanazopitia.

Swingewood (1975) anasema asili ya uhalisia ilitokana na kuwepo kwa tabaka la juu na maendeleo ya viwanda katika nchi za ulaya. Uzalishaji wa mali uliwasababisha baadhi ya wanajamii kunyanyaswa na hapo pakawa na haja ya kuyaangazia masuala yanayohusu jamii kwa uwazi. Kazi za kifasihi zilizoandikwa katika karne ya kumi na tisa zinahusishwa na uhalisia. Kazi hizi zilijihusisha na usawiri wa hali kama ilivyo katika jamii. Anaendelea kusema  kazi za kihalisia huangazia mabadiliko ya jamii kihistoria. Kwa mujibu wa haya, mwandishi anayehusishwa na uhalisia ana jukumu la kuangazia jamii kiwakati na kuonyesha mabadiliko ambayo jamii husika imepitia.

Msokile (1993) anaeleza kuwa uhalisia ulianza mwaka wa 1820. Msingi wa nadharia hii ni kuwa jukumu la fasihi ni kuusawiri ukweli wa jamii husika na vilevile mazingira yawasilishwe kama yalivyo. Nadharia hii pia inapendekeza wahusika katika kazi za kifasihi wawakilishe jamii halisi.Kwa hivyo kazi za fasihi kulingana na nadharia hii zinatarajiwa kuakisi masuala ya ulimwengu kama yalivyo bila ya kuzua uchangamano wowote katika kuelewa kazi hizo.

Hegel(1979) anaeleza kuwa kusudi la sanaa ni kutuwezesha kujua ukweli kuhusu maisha yetu kwa minajili ya kujielewa zaidi. Anaendelea kusema ya kuwa, hali ya maisha huwachochea wahusika katika kazi ya fasihi kutenda matendo fulani. Pia alipendekeza matumizi ya neno uhalisia katika fasihi ambazo zina wahusika wanaochochewa na hali ya maisha inayowazunguka kutenda vitendo fulani katika kazi husika. Kulingana na nadharia hii, kazi za kifasihi zina jukumu la kushughulikia masuala yanayomwathiri msomaji moja kwa moja bila ya kupiga chuku masuala haya. Mwandishi wa kazi za kifasihi basi lazima ajihusishe na mazingira yake pamoja na kuelewa hali ya jamii yake.

Wellek(1960) anaeleza uhalisia kama uwasilishaji wa hali halisi ya maisha ya jamii kama yalivyo katika kipindi fulani cha wakati.Uhalisia kwa hivyo haujihusishi na dhana ya udhahaniakazi za kifasihi zinatarajiwa kuwasilisha masuala yanayoikumba

jamii katika kipindi fulani cha wakati.Katika kufanya hivi, mwandishi atauzingatia uhalisia wa hali ya masuala hayo kiwakati.

Lukacs (1962) ni miongoni mwa wafuasi wa Karl Marx ambaye anahusishwa na nadharia ya uhalisia. Aliamini kuwa uhalisia ulistahili kusawiriwa kiukamilifu na pia taswira ya uhalisia inayoshughulikiwa ni lazima ichunguzwe kindani ili kueleza mabadiliko ya kiwakati katika jamii na visababishi vya mabadiliko haya. Anaendelea kueleza kuwa, mwandishi wa kiuhalisia anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kuidhihirisha mifanyiko ya mabadiliko iliyoko.

Hemming na wenzake (1978) wanaeleza kuwa, mwanahalisia hana budi kuangazia matukio kama yanavyotendeka katika kipindi fulani cha wakati. Mandhari ya kazi hizi pia yanahitajika kuwa ya kawaida na yanayoeleweka. Masuala yanayokumba jamii yanapasa kusawiriwa kwa njia ambayo inaeleweka. Kama wanavyoeleza jamii inaweza kuvutiwa na kazi ambazo zinazingatia na kuusawiri ukweli wa hali halisi ya maisha.

Kutokana na haya ni wazi kuwa wahusika katika kazi ya kifasihi wanahitajika kuwa viwakilishi vya jamii husika, kimaadili na hata waonyeshe picha halisi ya maovu wanayotenda wanajamii bila ya kuyapiga chuku. Uteuzi wa mandhari katika kazi ya fasihi pia ni muhimu. Uteuzi huu utamsaidia msomaji kukubali na kushawishiwa na yale yanayowasilishwa na mwandishi fulani wa kazi za fasihi. Ikumbukwe kuwa kadri wakati unavyobadilika, masuala ya jamii nayo pia hubadilika. Masuala yaliyoshughulikiwa katika enzi za kupigania uhuru, hayawezi kuwa sawa na masuala ya siku hizi. Kwa hivyo, mwandishi anayehusishwa na nadharia hii ya uhalisia inabidi naye pia abadilike kiwakati katika usawiri wa masuala ya kijamii.

Kulingana na Wamitila (2002) kazi zilizoandikwa katika mwelekeo wa nadharia hii, huwa na sifa ya matukio ya kweli yanayoiangazia jamii ya mwandishi. Kazi hizi basi huakisi hali ya maisha kama ilivyo. Wanauhalisia huwasawiri wahusika kama binadamu wa kawaida au viumbe wanaoeleweka au kuonekana katika jamii halisi. Matendo na maisha ya wahusika hawa ni halisi.Anaendelea kudai ya kwamba, msingi wa nadharia hii ni “usimulizi wa kimuhakati”. Usimulizi wa aina hii unasisitiza

masimulizi ya matukio kama yalivyo katika ulimwengu wa kawaida au pia ni usimulizi ambao una matukio yanayokaribiana na hali ilivyo katika jamii.

Licha ya kuwa nadharia hii husisitiza dhana ya ukweli kutumika katika usimulizi, mwandishi yeyote yule hana uwezo wa kusimulia matukio yote katika jamii yake.Yeye kwa hivyo huitathmini jamii yake kisha anachagua yale anayotaka kuyawasilisha kwa wasomi wa kazi yake. Uchaguzi huu huchochewa hasa na yale yanayomwathiri au kumkera mwandishi. Baadhi ya waandishi huonyesha msimamo wao kwa ufanya hivi kama njia ya kuyakemea maovu wanayoyaona katika jamii.

Mbatiah (2001) anafafanua dhana ya uhalisia kama istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi. Wasanii walioshughulikia nadharia hii waliamini kwamba ukweli uliweza kupatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za mwanadamu katika mandhari yake ya uhalisia. Mandhari kama yale hayana budi kusawiriwa bila kutiwa chumvi wala kudunishwa kwa njia yoyote ile.Wamitila (2003) anaeleza kuwa kuna aina mbalimbali za uhalisia katika fasihi.

Wamitila( aliyetajwa) anaelezea uhalisiajabu kama dhana iliyobuniwa na msanii wa ujerumani Franz Roh na inahusishwa na waandishi wa Marekani ya kusini na pia nchi zinazojulikana kama ulimwengu wa tatu. Uhalisiajabu huyaelezea matukio ya kiajabu au kifantasia kwa namna ya moja kwa moja. Mbatia (2001) anaueleza uhalisiajabu kama mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na mitindo ya uhalisiajabu inaelezwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida.

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza uhalisia wa kijamaa kuwa una misingi yake katika mawazo ya Kari Marx. Waasisi wa nadharia hii ni pamoja na Lukacs, Marxim Gorki miongoni mwa wengine. Anaendelea kusema kuwa nadharia ya uhalisia wa kijamaa hunuia kuonyesha jamii katika uyakinifu wake na huonyesha hatua zake za kimabadiliko.

Wamitila (aliyetajwa) anasema uhalisia wa kihistoria ni ule unaosisitiza usawiri wa jamii katika uhalisi wake wa kihistoria. Anaendelea kusema kuwa kilicho muhimu

katika aina hii ya uhalisia ni kuakisi hali ilivyo kihistoria bila ya kukiuka hali halisi ya historia.

Wamitila(2003) amefafanua uhalisia wa kirasimu kama uhalisia ambao unajifunga kwenye kanuni ya ushabikikweli na jitihada ya kuhakikisha yanayosimuliwa yanaafikiana na uhalisi kwa kiasi kikubwa. Ni uhalisia ambao hauna sifa zozote za matukio yasiyoweza kutendeka katika hali halisi.

Nadharia hii ya uhalisia ilitusaidia katika uchanganuzi wa kazi tulizozishughulikia za Leonard Sanja. Mwandishi huyu ameyaangazia maisha kama yalivyo katika hali halisi na hivyo basi kumwezesha msomaji kuuona ulimwengu kama ulivyo. Jamii katika kazi hizi inaonekana ikikabiliana na changamoto kama vile unyakuzi wa ardhi na ufisadi unaoendelezwa na viongozi dhalimu. Changamoto hizi ni sawa na zinazoshuhudiwa na mengi ya mataifa katika bara la Afrika.

Amewasawiri wahusika vijana kama wanyonge ambao wanakumbwa na changamoto si haba. Mandhari ambamo matukio yanatendeka ni ya kihalisia na ambayo yanaweza kubainika katika jamii tunamoishi. Baadhi ya matatizo ambayo jamii ya kazi tutakazoshughulikia ni pamoja na ukosefu wa huduma za kiafya, ukosefu wa maji safi ya kunywa na pia ukosefu wa ajira hasa kwa vijana. Masuala ambayo mwandishi huyu ameyaangazia ni sawa na hali ilivyo katika jami tunamoishi.Vijana wanatumia mbinu mbalimbali kukabiliana na viongozi dhalimu ili kutimiza azma yao ya kuleta utawala wa haki.Katika maisha ya hali ya kawaida, vijana wameibuka kuwa watetezi wa wanyonge katika jamii.

### 1.7.1 Mihimili ya nadharia ya Uhalisia

Nadharia ya uhalisia huhusishwa na mihimili ifuatayo:

(i) Mwandishi wa kazi ya kifasihi anastahili kuwasawiri wahusika wa kazi yake kwa hali ya uhalisia. Wahusika watende na wawaze kama jamii inavyotenda.

(ii) Uhalisia unatoa picha halisi ya maisha ya kawaida.

(iii) Fasihi ni kioo cha jamii kwa hivyo sharti kazi yoyote ile ya fasihi iiangazie jamii kama ilivyo.

(iv) Kila kizazi kina mtazamo tofauti kuhusu ukweli. Jinsi maisha yanavyobadilika, jamii nayo vilevile inabadilika. Ukweli wa jamii fulani huenda ukatafasiriwa visivyo na jamii nyingine.

(v) Kazi za kifasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisia. Kazi hizi zinasawiri hali halisi ya maisha katika jamii na kwa hivyo matukio katika kazi hizi yanawakilisha uhalisia ikiwa ni pamoja na mandhari.

Mihimili hii itatufaa kubaini yafuatayo katika utafiti wetu:
Mhimili wa kwanza utatusaidia kubaini iwapo wahusika katika kazi hii ni wa kidhahania au ni wa kihalisia kama mhimili huu unavyopendekeza.Mhimili wa tatu utatuwezesha kubaini iwapo katika uchanganuzi wa kazi hizi tutaweza kuona vijana katika hali ya kiuhalisia.Mhimili wa tano pia utatusaidia kujua iwapo kazi tutakazozishughulikia zinaakisi hali ya maisha kama yalivyo kwa kurejelea matukio na mandhari ambamo matukio yanatendeka.

## 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Mogambi (1983) ameangazia hali ya wanyonge hususan vijana kama inavyojitokeza katika riwaya tatu za S. Mohammed. Katika utafiti wake aliangazia dhuluma wanazopitia wanyonge katika maisha ya kila siku. Kazi hii ina uhusiano na utafiti wetu kwa kuwa vijana wakiwa miongoni mwa jamii wanapitia dhuluma hizi katika harakati zao za kujenga nchi. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa, vijana katika kazi za Leonard Sanja wanapitia dhuluma mbalimbali. Tofauti naye utafiti wetu ulijishughulisha na nafasi ya vijana katika ukombozi. Utafiti wetu uliangazia dhuluma dhidi ya vijana kama mojawapo wa vichocheo vya kupigania ukombozi .

Lugano (1989) ameangazia wahusika wa kike katika kazi za Kezilahabi. Kazi hii ilitufaa kwa kuwa wahusika wa kike wamechorwa kama viumbe duni na pia wao ni wanyonge. Amebainisha kuwa wahusika vijana wa jinsia ya kike wameonyesha jitihada ya kujikomboa kutoka kwa dhuluma wanazopitia. Utafiti huu ulitufaa tulipokuwa tunachunguza jinsi vijana wanachangia katika kuleta ukombozi. Pamoja na haya ni muhimu kutaja kuwa vijana wa jinsia ya kiume wamesahaulika na jamii ambayo imempigania kijana wa kike.

Karanja (1990) amezihakiki tamthilia za *Mzalendo Kimathi, Mkwava wa Uhehe* na *Kinjeketile.* Katika uhakiki wa kazi hizi, amebaini taswira yakinifu ya mwafrika katika vita vya ukombozi. Mtafiti huyu alionyesha jinsi mwafrika alihusika katika vita vya ukombozi. Utafiti huu ulitufaa kuelewa zaidi suala la ukombozi unaoletwa na vijana katika kazi teule. Utafiti wetu ulichunguza wahusika vijana katika kuikomboa jamii.

Kiango(1992) ameshughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Utafiti wake unadhihirisha udhalilishaji wa jinsia ya kike. Katika maisha ya sasa, vijana wa jinsia zote mbili wanakumbwa na changamoto mbalimbali na kwa hivyo ni jambo la muhimu kuangazia jinsia hizi zote mbili. Utafiti huu ulitupa mwanga wa dhuluma wanazopitia wanawake na hivyo zinakuwa kichocheo cha vijana kupigania ukombozi wa jamii nzima. Hata hivyo kuna haja ya kuwahusisha vijana wa jinsia zote katika ukombozi wa jamii. Pia kuna haja ya kutafuta suluhisho la matatizo wanayopitia vijana wote.

Wafula (1999) alizihakiki tamthilia tatu ambazo zina wahusika vijana. Tamthilia hizi ni pamoja na: *Wakati Ukuta* (1972), *Hatia* (1972), na *Uasi* (1980). Katika uchanganuzi wake, anatoa kauli muhimu sana anaposema vijana huweza kubadilika kwa urahisi kwa vile imani zao za kimsingi zinaendelea kujengeka. Hata hivyo uhakiki huo haukubaini kufaulu kwa vijana katika kuinasua jamii kutoka kwa matatizo yanayoikumba. Utafiti wetupamoja na kubainisha mchango wa vijana katika kuleta ukombozi, tulibainisha vile vile iwapo vijana watafanikiwa kuleta ukombozi wa jamii.Katika utafiti huu, ilibainika kuwa hali mbaya ya kiuchumi na kisiasa haikubadilika hata baada ya kuondoka kwa mkoloni. Hatimaye panakuwa na haja ya jamii kujikomboa kisiasa na kiuchumi. Katika utafiti wetu, tuliwaangazia vijana katika suala la ukombozi sio tu wa kisiasa na kiuchumi bali pia ukombozi dhidi ya dhuluma zote zinazoikumba jamii.

Kairu (2005) alishughulikia uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto. Alitumia nadharia ya uhalisia ili kubaini ni kwa kiasi kipi mwandishi anadhihirisha uhalisia na umuhimu wake katika fasihi ya watoto. Alichanganua maudhui, wahusika na mandhari kwa kutumia nadharia ya uhalisia akiwa na kusudi la

kuonyesha umuhimu wa uhalisia katika fasihi ya watoto. Utafiti huu una mwingiliano na utafiti wetu kwa kuwa sisi tulitumia nadharia hii ya uhalisia katika uchanganuzi wetu. Hata hivyo, tofauti ni kuwa yeye anashughulikia fasihi ya watoto huku sisi tukiongozwa na nadharia ya uhalisia kubaini nafasi ya vijana katika kuleta ukombozi.

Nkonge (2006) alichambua riwaya mbili, *Nguvu ya Sala* na *Kichwa Maji*. Katika utafiti wake alichunguza masuala mbalimbali kuhusu vijana kama vile mapenzi na ndoa, malezi na hata uozo wa jamii.Hata hivyo kuna haja ya kujiuliza ni jinsi gani vijana watakombolewa kutoka kwa changamoto hizi zinazowakabili. Utafiti wetu ulijaza pengo hili kwa kubaini majukumu ya vijana katika kuleta ukombozi wa jamii nzima.

Mutua(2007) ametafiti kuhusu mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili ambazo ni *Natala*(1997), *Kitumbua Kimeingia mchanga* (2000) na *Migogoro*(2006). Kazi hii ilitusaidia tulipokuwa tukiangalia jinsi au mchango wa vijana katika juhudi za kuleta ukombozi katika jamii. Tofauti na huu utafiti wetu ulilenga vijana kama viungo muhimu vinavyoleta ukombozi wa jamii nzima ikiwepo ukombozi wao wenyewe na vijana wenzao. Kazi tulizozishughulikia ni kutoka tanzu zote tatu tofauti na Mutua ambaye alishughulikia utanzu wa tamthilia.

Kiongera ( 2010) ameshugulikia mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthlia nne za Kiswahili.*Maua Kwenye Jua La Asubuhi* (2006), *Kifo Kisimani*(2001), *Pengo*(2003), na *Seserumbe*. Mtafiti huyu alijishughulisha na mabadiliko waliyoleta vijana katika kazi hizi. Baadhi ya mabadiliko wanayoleta vijana yanachangia kufanikisha ukombozi. Kiongera katika utafiti wake ameonyesha kuwa vijana wanatambua maovu ya viongozi wa kisiasa na hata matatizo mengine ya kijamii kama vile kudhulumiwa kwa wanawake. Tofauti na utafiti wetu, Kiongera alijishughulisha na kazi za waandishi wawili tofauti huku nasi tukihakiki kazi za mwandishi mmoja. Utafiti wetu ulijikita katika aina mbalimbali za ukombozi zinazoletwa na vijana na pia uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Kazi tunazochunguza pia ni kutoka tanzu zote za fasihi andishi.

Naliaka (2012) ameangazia hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara* .Mtafiti huyu ameangazia hali chanya na hasi za vijana katika riwaya hii. Kazi hii itatufaa kwa kuwa mtafiti amechunguza vijana kwa misingi ya changamoto zao maishani hali kadhalika nafasi chanya ya vijana katika jamii. Utafiti wetu una uhusiano na huu kwa kuwa vijana pamoja na jamii nzima katika kazi tunazochunguza wanapitia changamoto za aina hii na ni kutokana na haya ndipo vijana wanakuwa katika mstari wa mbele kupigania ukombozi wa jamii zao. Baada ya kubaini changamoto zinazowakabili vijana, kuna haja ya kutafuta suluhisho la hali hiyo. Haya yalishughulikiwa na utafiti wetu.Tofauti na utafiti huu, utafiti wetu pia ulihusu tanzu zote tatu za fasihi katika kubainisha umuhimu wa vijana katika suala ukombozi.

Obure (2012) ameshughulikia dhuluma ya vijana wa kike katika riwaya mbili *Rosa Mistika* na *Tumaini*. Utafiti wake ulijihusisha na vijana wa jinsia ya kike pekee, tofauti na utafiti wetu ambao ni wa vijana wa jinsia zote. Pia utafiti wetu ulichunguza tanzu tatu za mwandishi mmoja. Tofauti na mtafiti huyu, utafiti wetu uliangazia uwezo wa vijana katika kujikomboa dhidi ya dhuluma wanazopitia.

Nyamwemba (2012) ameangazia uchanganuzi linganishi wa maswala ya vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na waandishi katika *Diwani ya Tunu Za Ushairi.* Katika utafiti wake, mwandishi ameshughulikia changamoto wanazopitia vijana suala ambalo linakaribiana na utafiti tutakaoushughulikia. Mtafiti huyu alichunguza mashairi tofauti na kazi yetu ambayo ilichanganua riwaya, tamthilia na hadithi fupi, ambazo ni kazi za mwandishi mmoja.Utafiti wetu pia uliangazia changamoto hizi ambazo zinawasukuma vijana kupigania ukombozi wa jamii.

Kipyegon (2013) aliangazia nafasi na utambulisho wa mwanamke katika N*atala na kifo Kisimani* ili kubainisha juhudi za mwanamke katika kujikomboa na kupata hadhi katika jamii husika. Utafiti huu unafanana na utafiti wetu tutakapokuwa tunaangazia suala la ukombozi. Hata hivyo kuna haja ya kuwazindua vijana wote bila kuzingatia jinsia zao ili kuhakikisha jamii yote imejikomboa. Vijana kama viungo muhimu katika jamii wanahitaji kupewa nafasi sawa katika majukumu ya jamii.

Wanjiru (2013) alifanya utafiti kuhusu uhalisia na uhalisia ajabu katika *Babu alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Katika utafiti wake aliangazia wahusika, mandhari

na matukio ya uhalisia na uhalisia ajabu katika kazi hizi. Uhalisia ulibainika katika kazi zilizotafitiwa ikiwa ni pamoja na matendo ya baadhi ya wahusika.Kwa hivyo tafiti huu unahusiana na utafiti wetu kwa kuwa tuliongozwa na nadharia hii ya uhalisia kubaini nafasi ya vijana ya kuleta ukombozi katika kazi za Leonard Sanja. Hata hivyo kuna haja ya kujikita katika kipengele kimoja ili kuweza kuwa na uchanganuzi wa kina. Hii ndio maana utafiti wetu utajishughulisha na wahusika vijana pekee

Lomatoro (2014) alichunguza viwango vya uhalisia na ubunifu katika *Cheche za moto* na *Kaburi bila Msalaba* kwa kutumia nadharia ya uhalisia. Katika utafiti wake, alitumia vigezo mbalimbali ili kubaini uhalisia katika kazi hizi. Vigezo hivi ni pamoja na visa, matukio na mandhari. Mtafiti alionyesha jinsi kazi hizi zinaonyesha yale yanayofanyika katika nchi za kiafrika na kwa hivyo kusawiri uhalisia. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa tulitumia nadharia ya uhalisia kubaini jinsi mwandishi amefaulu kuwasawiri wahusika vijana kihalisia kwa kurejelea jukumu lao la kujikomboa kutokana na changamoto zinazowakumba. Kusudi la mtafiti huyu lilikuwa kubaini jinsi uhalisia unajitokeza katika kazi hizo. Utafiti wetu ulikuwa tofauti na wake kwa kuwa, sisi tulijikita hasa katika usawiri wa wahusika vijana kihalisia katika kazi za mwandishi mmoja.

Mwazani (2015) alifanya utafiti kuhusu maudhui ya ukombozi katika *Diwani ya Jicho la Ndani*. Katika utafiti huu alifafanua dhana ya ukombozi na aina mbali mbali za ukombozi katika diwani hii. Hata hivyo utafiti wetu haukuhusu utanzu wa ushairi na pia ulichunguza nafasi ya vijana katika kuleta ukombozi huu.

Ndanu (2016) alichunguza maudhui ya ukombozi katika *Wimbo mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Katika kazi hii yake ameangazia changamoto zinazowakumba wananchi na pia aina mbalimbali za ukombozi. Baadhi ya changamoto hizi ni vichocheo kwa wahusika vijana katika kazi tulizochunguza .Ili ukombozi wa jamii ufaulu, kuna haja ya kuwahusisha vijana katika suala hili nzima la ukombozi kwa kubaisha majukumu yao muhimu katika jamii. Hii ni pamoja na ukweli kuwa vijana ni viungo muhimu sana katika ujenzi wa jamii mpya huru. Kuna haja pia ya kuangazia ukombozi wa

vijana. Kwa hivyo utafiti wetu ulikuwa tofauti na huu kwa kuwa tulichunguza nafasi ya vijana katika suala la ukombozi wa jamii nzima

Muriithi (2016) alitafiti kuhusu changamoto zinazowakumba vijana katika riwaya ya *Upotevu* na Dunia *uwanja wa Fujo*. Utafiti huu uliangazia changamoto za aina mbalimbali zinazomtatiza kijana. Utafiti huu ulitufaa tulipokuwa tukibainisha vichocheo vya maisha na jinsi vimekuwa vichochezi kwa vijana kuleta ukombozi.Utafiti huu unatofautiana na utafiti wetu kwa kuwa alitafiti changamoto zinazowakumba vijana ilhali sisi tulichunguza mchango wa vijana katika kujikomboa kutokana na changamoto hizi.

Kihara (2016) alichunguza nafasi ya vijana katika riwaya za *Pendo La Karaha* na *Kovu Moyoni.* Utafiti huu ulihusu nafasi chanya na nafasi hasi wanazopewa vijana katika kazi hizi za kifasihi. Baadhi ya nafasi ambazo ameangazia zilitufaa katika utafiti wetu.Tulipokuwa tunachanganua matatizo wanayopitia vijana wanapopigania ukombozi. Utafiti wetu ulitofautiana na huu kwa kuwa, sisi tulichunguza tanzu tatu za kifasihi na vilevile nafasi ya vijana katika ukombozi.

**1.9 Njia za utafiti**

Utafiti wetu ulikuwa wa kimaktaba. Katika maktaba, tulisoma kazi tulizoziteua ambazo ni:Tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*(2011) , hadithi fupi ya "Mwavyaji wa Roho" *(*2011) katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho* na hadithi nyingine pamoja na riwaya *Yasinya* (2014). Tulisoma kazi hizi tatu kwa kusudi la kudondoa na kutathmini nafasi ya vijana katika ukombozi wa aina mbali mbali.

Pamoja na kwamba mtindo wa uwasilishaji ni tofauti katika kila utanzu, utafiti wetu ulidhamiria kuchunguza mwelekeo wa kifalsafa wa mwandishi huyu katika kazi tatu hizi kuhusiana na nafasi ya vijana katika kuleta ukombozi wa aina mbalimbali.

Mbali na kusoma kazi hizi tulisoma kazi mbalimbali ambazo zimehakikiwa kwa msingi wa nadharia ya uhalisia zikiwemo vitabu, makala, na hata tasnifu. Kazi hizi zilitufaa kwa kuwa tulikuwa na uelewa mpana kuhusu nadharia ya uhalisia ambayo tuliitumia kuzichanganua kazi hizi. Vile vile tulisoma kazi zingine zilizohusu maswala ya ukombozi kwa kusudi la kuweza kufafanua swala hili la ukombozi

kulingana na wasanii mbalimbali.Data ya utafiti tuliyoipata kwa kusoma vitabu tulivyoteua ilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya uhalisia ambayo ilitusaidia kubaini mchango wa vijana katika kuleta ukombozi.

Mihimili ya nadharia hii ilituongoza katika kuangazia uhalisia wa vijana katika mazingira yanayotuzunguza huku tukilinganisha na ulimwengu wa kifasihi katika kazi tulizoshughulikia. Aidha tuliongozwa pia na malengo ya utafiti wetu. Baadaye, matokeo ya utafiti wetu yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na kiufafanuzi katika sura mbalimbali.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza, tulieleza mada ya utafiti wetu na pia mwelekeo wa utafiti huu tukiongozwa na malengo ya utafiti.  Nadharia tuliyotumia ni nadharia ya uhalisia ambayo hujikita katika kueleza masuala kwa njia ya ukweli kama ilivyo katika hali halisi. Masuala mengine ambayo yalishughulikiwa katika sura hii ni: upeo na mipaka ya utafiti wetu, sababu ya kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada na kisha tukaeleza njia tutakazotumia katika utafiti wetu.

# SURA YA PILI

# UKOMBOZI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii ya pili itashughulikia mambo yanayochochea haja ya kuwepo na ukombozi katika jamii kupitia kwa fasihi. Kama wanavyoeleza Kimani Njogu na Chimera (1999) fasihi ni sanaa inayowasilisha hali, maingiliano,mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake.Wanaendelea kusema fasihi kwa hivyo inachukuliwa kama chombo kimojawapo kinachomsaidia binadamu kuyaelewa mazingira yake na hivyo basi ni zana muhimu ya kumkomboa mja kutokana na madhila yaliyosababishwa na waja wenziwe au na maumbile makali.

Ni kutokana na haya ambapo wasanii wa kazi za kifasihi za Kiswahili wana jukumu kubwa la kuwazindua wanajamii kupitia kazi zao ili waweze kuona hali ya maisha kama ilivyo. Fasihi ina jukumu la kushughulikia masuala yanayoizunguka jamii kupitia kwa maudhui. Kwa kuwa fasihi ni kioo cha jamii, mwandishi hujibidiisha kuifahamu jamii yake na kisha kuwasilisha yale yanayoikumba kupitia kwa kazi ya kifasihi. Kusudi la fasihi linaweza kuwa kuelimisha, kukashifu, kuadilisha au hata kupongeza.

Jamii inapokumbwa na maonevu fulani inakuwa na msukumo wa kupigania haki zake ili kujikomboa kutoka kwa hali hii. Ili kuelewa maonevu haya sura hii itaichunguza jamii katika awamu tatu ambazo ni Afrika ya kale, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Swingewood (1975) anaendelea kusema kuwa kazi za kihalisia huangazia mabadiliko ya jamii kihistoria. Kwa mujibu wa haya mwandishi anayehusishwa na uhalisia ana jukumu la kuangazia jamii kiwakati na kuonyesha mabadiliko ambayo jamii husika imepitia.

Kwa hivyo awamu tatu hizi zitatupa msingi wa kuelewa hatua mbalimbali ambazo jamii imepitia na ambazo zimeipa msukomo wa kutaka kujikomboa kutokana na udhalimu wa kiuchumi, kisiasa na hata kiutamaduni.

## 2.1 Afrika ya Kale

Kabla ya ujio wa wageni katika bara la Afrika, waafrika walishuhudia utulivu mwingi wakiongozwa na viongozi wao kulingana na tamaduni zao. Jamii ziliishi pamoja na kufurahia utangamano miongoni mwao huku wakiendeleza biashara za kubadilishana bidhaa zao. Karanja (1990) akirejelea tamthilia ya *Mukwava wa Uhehe* anaeleza kuwa waafrika walikuwa wenye ustaarabu uliojitosheleza. Walikuwa wameunganika chini ya viongozi wao kama Mukwava wa Uhehe .Waafrika vilevile walikuwa na itikadi , imani na miiko yake.

Ilikuwa si kawaida kushuhudia maovu yanayoendelezwa na viongozi wa baada ya uhuru. Machafuko yaliyoshuhudiwa yalikuwa kama vile ya wizi wa mifugo kati ya jamii zilizopakana. Hata hivyo hali hizi zilitulizwa na viongozi katika jamii hizi na hatimaye utulivu ulirejea. Kila jamii ilijishughulisha na shughuli zake za uzalishaji mali kama vile ukulima, uvuvi, uwindaji na hata biashara za kubadilishana vyakula. Bara la Afrika lilikuwa na rasilimali nyingi ambazo licha ya kuwa waafrika hawakuwa na maarifa mengi kuzihusu, rasilimali hizi ziliwafaidi waafrika kwa kiasi kikubwa. Waafrika hawakuwa na migawanyo ya kidini ila tu kila jamii ilikuwa na njia zake za kuabudu ambazo ziliwaridhisha.

Hali hii ya utulivu inadhihirishwa na kazi za kifasihi katika kipindi hiki. Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kwamba kazi za kwanza katika fasihi andishi ya Kiswahili zilikuwa ni mashairi yaliyotungwa sehemu za Lamu nchini Kenya.Maudhui makuu katika kazi hizi yalikuwa ni ya kidini hasa dini ya kiislamu. Hii ina maana kwamba mambo muhimu katika kipindi hiki yalikuwa yanahusu imani za kidini kwa kuwa hapakuwepo na hali za unyanyasaji ambazo zingeangaziwa na waandishi hawa.

Baadhi ya kazi hizi za kifasihi katika kipindi hiki zilikuwa za kuburudisha, na hata kuhusu maadili ya jamii. Nyingi za kazi hizi ilikuwa ni fasihi simulizi hasa ushairi simulizi. Kila jamii ilikuwa na fasihi yake ambayo ilioana na shughuli zake za uzalishaji mali hali kadhalika shughuli nyinginezo za kijamii.

## 2.2 Kipindi cha ukoloni

Kimani Njogu(1997) akimnukuu Brett (1972) anaeleza ukoloni kama mfumo wa utawala unaopora haki na kuwagandamiza watu wengine. Hatimaye watawaliwa hushindwa kujitegemea kiuchumi na hata kisiasa. Woddis (1972) naye anaeleza ukoloni kama mfumo ambao nchi moja huikandamiza nchi nyingine na kutwaa madaraka ya kutawala ili iwanyonye wenyeji kikamilifu. Kutokana na haya tunaweza kusema ukoloni ni hali ambapo taifa moja huiteka nchi nyingine kwa kuchukua mamlaka ya kisiasa, kiuchumi na hata kiutamaduni kwa manufaa yao wenyewe.Miongoni mwa wageni ambao waliingia katika bara la Afrika ni Warumi, Wareno na hata Waarabu. Hawa walikuja na lengo la kutalii nala kibiashara. Katika safari zao, wageni hawa waligundua kuwa bara la Afrika lilikuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali ambazo zingewafaidi.

Biashara iliyoendelezwa na waarabu kwa kiwango kikubwa ilikuwa ni biashara haramu ya pembe za wanyama wa pori na hata ngozi za baadhi ya wanyama kama vile chui na simba. Hatimaye biashara ya watumwa iliendelezwa na waarabu pamoja na baadhi ya waafrika. Kazi za kifasihi kama vile *Uhuru wa Watumwa* ya James Mbotela(1934) inadhihirisha jinsi waarabu walinufaika na rasilimali za Afrika kupitia kwa biashara haramu. Mbotela(aliyetajwa) anaeleza kuwa katika misafara ya wanabiashara hawa, baadhi ya watumwa walijikomboa kutoka mikononi mwa mabwana kwa kutoroka. Hapa palikuwa na haja ya kazi za kifasihi ambazo zingekuwa na maudhui ya ukombozi wa mwafrika dhidi ya dhuluma ambazo alikuwa anapitia kutoka kwa wageni hawa na hata waafrika wasaliti.

Hatimaye waingereza walianza kuingia barani Afrika na kueneza dini ya Kikristo kupinga ile ya kiislamu ambayo ilikuwa imeenezwa na Waarabu. Hapo ndipo waafrika walianza kukengeuka na kubadilisha mitazamo yao kuhusu utamaduni wa kiafrika na hata imani zao za kidini. Mfumo huu wa ukoloni uliendeleza dhuluma nyingi kwa waafrika ambazo ziliwachochea kupigania ukombozi hasa wa kisiasa.

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa lugha ya Kiingereza na fasihi yake ni vyombo vya ukandamizaji na ulazimishi wa lugha ya kimagharibi kwa mataifa yaliyotawaliwa pia ni juhudi ya kutweza mchango wa mataifa yaliyotawaliwa katika

kuelewa na kueleza mazingira yake. Kwa hivyo ili kuwapumbaza waafrika, wakoloni waliwaonyesha waafrika kuwa utamaduni wao ulikuwa ni ushenzi na kwa hivyo kuwarai wakumbatie mafunzo ya kigeni. Ngugi wa Thiong'o (1986) pia anazungumzia suala hili la ulazimishaji wa lugha ya Kiingereza katika mataifa ya kiafrika. Anaendelea kusema kuwa hii ilikuwa njama ya kutupilia mbali tamaduni za kiafrika. Lugha hii ilitumika katika elimu na kwa hivyo kuwafunza watoto wa Kiafrika tamaduni za Uingereza. Kama anavyoeleza Ngugi utawala wa kiuchumi na kisiasa hauwezi kuwepo bila ya utawala wa kitamaduni. Kwa hivyo waingereza walitumia mbinu hii ili kuendeleza utawala wao barani Afrika. Wengi wa waafrika walipata elimu ya kimagharibi na hapo wakaanza kumwonea mwingereza fahari.

Wakoloni waliingia katika nchi za Afrika na kuanza kutawala katika nyanja mbalimbali kama vile za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Wageni hawa waliwanyanyasa wenyeji pamoja na kuchukua rasilimali zao. Suala la ukoloni limeangaziwa na kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili. Wakoloni walipofika barani Afrika, walijinyakulia sehemu ambazo walijua zitakuwa za manufaa kwao katika kilimo na hata biashara. Sehemu hizi ni kama vile bonde la ufa na hata pwani ya Afrika mashariki.

Waafrika hawakuruhusiwa kuendeleza kilimo ambacho kingewanufaisha kwa mfano hawakuruhusiwa kupanda mimea kama vile chai au kahawa. Haya yote yalikuwa kwa manufaa ya wakoloni ili waafrika wazidi kuwategemea wakoloni. Wengi wa waafrika walikuwa wafanyakazi nyumbani mwa wakoloni ambapo dhuluma iliendelezwa na wakoloni hawa na kuwaona waafrika kama kitu kisicho na dhamani. Baadhi ya waafrika walifanya kazi ngumu malipo yakiwa duni au pengine kupatiwa vyakula badala ya mishahara. Licha ya changamoto hizi waafrika waliendelea kuwaabudu wakoloni na kuwaona kama miungu. Dhuluma za ubakaji wa wanawake na wasichana wachanga zilisheheni katika kipindi cha ukoloni.Walibora(2012) anadhihirisha haya katika *Kidagaa Kimemwozea* ambapo waafrika katika maeneo ya Sokomoko hawakuruhusiwa kufuga ng'ombe wa maziwa bali wale wa kienyeji tu. Mbatia(2016) anasema kwamba baadhi ya mambo yaliyowaudhi waafrika zaidi katika kipindi hiki ni kilimo cha pamba ambacho kilikusudia kuwafaidi wajerumani.Waafrika hawakufaidika licha ya kuwa wao ndio walikuwa wakifanya kazi ngumu.

Ubaguzi wa  uliendelezwa na wakoloni katika baadhi ya mataifa ya Afrika kwa mfano, waafrika walitozwa kodi ya kiwango cha juu huku wakilipia huduma zote ambazo walizipata. Kwa upande mwingine wakoloni hawakulipia huduma hizi. Waafrika pia hawakukubaliwa kunufaika na baadhi ya huduma kama ilivyokuwa kwa wakoloni. Ubaguzi mwingine ulidhihirika katika asasi za kijamii kama vile elimu. Waafrika walitengwa na wana wao hawakuruhusiwa kupata elimu pamoja na wana wa wakoloni. Mfumo wa elimu katika shule za wakoloni vile vile ulikuwa tofauti na ule wa shule zilizohudhuriwa na waafrika. Licha ya haya, lugha za kiafrika zilichukuliwa kuwa duni na kwa hivyo wakoloni wakasisitiza waafrika wafundishwe lugha zao. aya yanadhihirishwa na Ngugi(1981) anaposema, elimu ya kigeni ilikuwa ikiwabagua waafrika kwa kuwa ilidhihirisha chuki nyingi dhidi ya majina ya kiafrika, mazingira yao na hata lugha yao.

Kupitia kwa dini ambayo ilikuja na wakoloni, utamaduni wa waafrika ulidunishwa na kupingwa na wakoloni. Mwafrika alishawishiwa kuwa utamaduni wake ulikuwa ni ushenzi kwa mfano katika *Uhuru wa Watumwa* ya Mbotela(1934), waafrika walikomeshwa kucheza ngoma za kiafrika na badala yake wakafunzwa mitindo mpya ya kimagharibi ambayo waliikumbatia. Kwa kufanya hivi wakoloni walifaulu kuwatawala waafrika na kujinufaisha wao wenyewe huku wakidai kuwa wamewaletea waafrika ustaarabu. Waafrika waliridhi baadhi ya tamaduni za kigeni na kuasi nyingi ya tamaduni zao.

Ukoloni uliendelezwa vilevile na baadhi ya waafrika waasi ambao walikuwa vikaragosi wa wakoloni wa kimagharibi. Kupitia kwa waafrika hawa, wakoloni waliwaelewa waafrika vyema na hata kujua siri zao. Vikaragosi hawa walipewa vyeo na wakoloni hawa ili wawasaidie kuendeleza utawala wao. Hawa walitumika kuwadhulumu waafrika wenzao na hata kuwasaliti. Kutokana na ukengeushi wa waafrika, wengi  walionea fahari masomo ya nchi za kimagharibi na kwa hivyo baadhi yao walienda ulaya na uingereza kupata masomo zaidi. Baadhi yao walirejea nyumbani ilhali wengine walikatalia ughaibuni.  Mauaji mengi yalishuhudiwa katika kipindi hiki cha ukoloni.Waafrika ambao walijaribu kutetea haki zao, waliuawa au kuwekwa gerezani.

Ni kipindi ambacho waafrika walinyimwa haki zao na pia hawakuwa na uhuru wa kutoa mchango wowote katika uongozi. Haya yanadhihirishwa na Karanja (1990) katika uchambuzi wa tamthilia za kiukombozi. Kwa hivyo waafrika walijitambua na hapo ndipo waliungana ili kupigania uhuru wao kama anavyoeleza Ngugi wa Thiong'o (1986) kwamba yeye na wahadhiri wengine kama vile Owuor Anyumba, Taban Lo Liyong walipinga kwa pamoja ufundishaji wa fasihi ya uingereza pekee katika elimu na badala yake wakapendekeza fasihi ya kiafrika na mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu ijumlishwe ili waafrika wauone ulimwengu kama ulivyo hapa Afrka, kwa kuwa Waingereza walilazimisha matumizi ya lugha ya kiingereza katika mfumo wa shule na kuwanyima wenyeji ubora lugha ya kutoka mazingira yao. Wanafunzi wa kiafrika vile vile waliadhibiwa kwa kuzungumza lugha zao za kienyeji.

Nadharia ya uhalisia inasisitiza uwasilishaji wa fasihi kwa njia ya ukweli na inayoweza kuthibitika. Kulingana na utafiti huu, ukoloni ni tukio la kihalisia barani Afrika ambalo linaweza kuthibitishwa ikikumbukwa kuwa athari za ukoloni zingali na athari kubwa hapa Afrika. Ni kutokana na changamoto hizi ambapo haja ipo ya kushughulikia ukombozi dhidi ya ukoloni katika mataifa ya bara la Afrika

**2.3 Baada ya Uhuru**

Baada ya waafrika kupigania uhuru wao, wakoloni walirudi kwao na hapo waafrika wakaanza kujitawala. Kipindi cha baada ya uhuru vilevile kilikumbwa na changamoto za aina mbalimbali ambazo ziliangaziwa katika kazi nyingi za kifasihi. Kutokana na uhuru waliokuwa nao waafrika, kipindi hiki kilishuhudia maandishi mengi ya kazi za kifasihi anbazo zilikusudia kupinga uongozi mbaya uliokuwa unaendelezwa na waafrika pamoja na wakoloni na kwa hivyo kupigania ukombozi wa pili. Licha ya waafrika kupata uhuru, waliendelea kukumbwa na changamoto anuwai ambazo ziliwachochea kupigania haki zao. Changamoto zilizowasukuma waafrika katika kipindi hiki ni pamoja na: ukoloni mamboleo, uongozi mbaya, umasikini, ukosefu wa haki na hata utabaka.

### 2.3.1 Ukoloni Mamboleo

Karanja (1990) anasema ukoloni mamboleo ni ile hali ya wakoloni kuendelea kuwanyanyasa na kuwadhulumu waafrika kwa kuwatawala kupitia kwa tabaka la vibaraka waafrika. Anaendelea kusema kuwa baada ya uhuru mwafrika anaendelea kunyanyaswa kupitia asasi mbalimbali zenye misingi ya kiuchumi kama vile siasa, biashara, dini na hata utawala. Akimnukuu Ngugi wa Thiong'o (1981) anasema kuwa ukoloni mamboleo ni hali ya kuendelea kunyonya malighafi na nguvu za wafanyakazi wa Afrika kunakofanywa na mfumo wa kimataifa wa kibepari kupitia uundaji na utimizaji wa mifumo dhaifu ya kiuchumi ya kibepari inayowafaa ambayo inasimamiwa na inaongozwa kwa niaba yao. Ukoloni mamboleo bado unaendelewa kushuhudiwa sio tu katika Afrika bali pia katika mataifa mengine hasa yale ya ulimwengu wa tatu.

Kwa maoni yetu Ukoloni mamboleo ni hali ambayo ingawa wakoloni walirudi makwao na kukomesha utawala wao, bado nchi huru zinazidi kudhibitiwa na mataifa ya kimagharibi kupitia kwa njia kama vile elimu, mfumo wa kiuchumi au hata kisiasa. Ukoloni mamboleo ni tukio halisi katika nchi za Afrika baada ya kupata uhuru. Ukoloni mamboleo ni tatizo ambalo limekita mizizi barani Afrika hata baada ya mataifa haya kujinyakulia uhuru. Athari kubwa na ambayo inaweza kuthibitishwa ni matumizi ya lugha za wakoloni kama vile Kiingereza, Kijerumani na hata Kifaransa. Kiingereza kinatumika kwa sasa kama lugha rasmi katika mataifa ya Kenya, Uganda na hata Tanzania. Kazi za kifasihi zimekuwa zikiangazia suala hili kwa kina na kwa hivyo pana haja ya kutafuta suluhu.

Hali hii hujitokeza kupitia kwa njia kadha wa kadha kwa mfano nchi za Afrika kuwekewa masharti yanayoambatana na misaada wanayopewa na nchi hizi za kimagharibi. Masharti haya ni kwa manufaa ya wakoloni ambao bado wanaendelea kudhibiti mataifa ya Afrika. Hatima yake ni kuwa nchi hizi zinaishia kuifilisi Afrika kwa madai eti wao ndio wafadhili. Mataifa haya ya kimagharibi yanafikia hatua hata ya kupendekeza kupunguzwa kwa wafanyakazi ili ufadhili wao udumu.

Nchi za kiafrika zinapokabiliwa na tatizo hili, hazina budi kuendelea kutegemea misaada kutoka nchi za kimagharibi na kujipata wakiziabudu nchi hizi. Wakoloni

wangali wanatoa mwongozo wa mipango ya kimaendeleo katika nchi za Afrika kwa mfano ujenzi wa barabara au hata reli. Hali hii inapotokea, mataifa yenye uwezo ndiyo yanayopata kandarasi za ujenzi licha ya kuwa bado kuna waafrika ambao wamehitimu katika nyanja hizi lakini ukosefu wa uwezo wa kiuchumi unakuwa kikwazo kikubwa. Ukoloni mamboleo umeendelea kuzinyonya rasilimali za bara la Afrika kwa madai ya kuzipatia misaada hali ambayo imesababisha umasikini  wa bara hili.Ukoloni mamboleo huendelezwa kupitia kwa asasi za kimataifa na mashirika mengine ambayo huungana ili kujinufaisha. Arege (2009) anadhihirisha haya anapoangazia tatizo la utegemezi na athari zake katika kupunguza kasi ya maendeleo katika nchi changa za kiafrika.

### 2.3.2 Uongozi Mbaya

Mataifa mengi katika bara la Afrika yanaendelea kukumbwa na changamoto ya uongozi mbaya ambao unaendelezwa na waafrika ambao wako katika uongozi. Baada ya nchi za bara la Afrika kujinyakulia uhuru, viongozi waliochukua mamlaka walikosa kuwajibika na badala yake wakaendeleza uongozi wa kidhalimu kama ulioshuhudiwa enzi za wakoloni.

Njoroge ( 2014) anaeleza uongozi mbaya kama hali ya kuongoza watu kidkteta bila kujali sheria au kanuni zinazotawala nchi fulani. Viongozi wa aina hii hutenda kama wapendavyo. Kwa hivyo tunaweza kusema uongozi mbaya ni hali ya viongozi kutawala nchi zao kwa manufaa yao wenyewe bila ya kujali maslahi ya wananchi waliowaweka mamlakani. Uongozi huu hudhihirisha hali ambapo wachache wananufaika huku wengi wakiendelea kuumia na kunyanyaswa hali ambayo husababisha mgawanyiko katika jamii au utabaka.

Were (1983) anaeleza kuwa uhuru wa kisiasa kutoka mikononi mwa wakoloni barani Afrika, ulikuwa na maana mbalimbali miongoni mwa waafrika wenyewe. Wengi wa wale walipigania uhuru walichukulia huu kama mwanzo wa maisha mapya yenye fanaka na uhuru wa kujitawala. Kulingana nao, uhuru ulikuwa ishara ya ukombozi kutoka kwa dhuluma walizokuwa wanapitia katika utawala wa mkoloni. Baadhi ya matarajio yao yalikuwa kwamba bara la Afrika lingekuwa na huduma bora za afya, masomo na hata usalama wa wananchi wake. Kwa upande mwingine kuna wale

ambao waliona hiyo kama fursa yao ya kuchukua nafasi ya wakoloni ili waweze kujinufaisha pamoja na jamaa zao. Anaendelea kusema kuwa,si ajabu kuwa hata baada ya uhuru haki za waafrika zimeendelea kukiukwa kila uchao hata baada ya viongozi kuahidi Afrika huru isiyo na mapendeleo.

Baadhi ya mambo ambayo hudhihirisha uongozi mbaya ni kama vile kubadilishwa kwa vipengele vya katiba ili kuwafaidi walio katika mamlaka. Haya si mambo mageni hapa barani Afrika ambapo baadhi ya viongozi wamekatalia uongozini na kuwanyima wengine nafasi ya uongozi.Were (aliyetajwa) anaeleza uongozi mbaya kama chanzo cha maovu ambayo yamerithishwa mataifa ya bara la Afrika na ambayo yamesababisha ukosefu wa maendeleo ya mataifa haya. Mataifa ya aina hii vile vile huwa na sifa za viongozi wenye wanaongoza kwa kimabavu hali ambayo husababisha kuadhibiwa kwa wale ambao wanapinga au kutokubaliana na uongozi huu.

Akimnukuu Forje J.W (1980) Were anasema licha ya kuwa Afrika ni bara ambalo lina utajiri mwingi wa madini dunia nzima, bara hili ndilo lenye umasikini mkubwa na pia ambalo halijaendelea likilinganishwa na mabara mengine. Haya yote yanahusishwa na uongozi mbaya katika bara hili. Uongozi mbaya kwa hivyo unaweza kuhuhusishwa na hali zifuatazo na ambazo huchochea wananchi kuungana ili kupigania haki zao ili wapate kujikomboa.

#### 2.3.2.1 Ufisadi

Were (1983) anaeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mamlaka katika afisi ya serikali na za kibinafsi. Ufisadi unahusishwa na utozaji wa milungula ili kumpa mtu huduma fulani na ambazo zinastahili kuwa za bure kwa umma.

Pia ni kule kujipatia mali au kuwezesha hali fulani kufaulu au kufanikiwa kwa kutumia njia za mkato na zisizo za kimaadili kama ushawishi wa hela, mapendeleo ya kinasaba, kikabila au hata msukumo wa cheo kwa kusudi la kujinufaisha. Ufisadi ni moja wapo wa njia za kupata mapato kupitia kwa njia isiyo ya haki. Ufisadi wa viongozi huhusishwa na utumiaji mbaya wa mamlaka hasa katika ofisi za umma au za kibinafsi kwa kusudi la manufaa ya mtu binafsi au kundi fulani la watu. Ufisadi hudhihirika wakati raia wanakosa kupewa huduma inavyotakikana katika asasi

mbalimbali za jamii kama vile mahakamani, hospitalini, shuleni na hata katika vituo vya polisi.

Njoroge (2014) akiwanukuu Ronald na Simpkins (1964) anasema umasikini ndio chanzo cha kuenea kwa ufisadi pamoja na ukosefu wa desturi zinazofaa hasa miongoni mwa viongozi wa kiafrika. Ufisadi pia huhusishwa na tabia ya ukarimu na kupeana zawadi wakati viongozi hawa wanataka kufaidika kwa njia nyingine ikiwa ni pamoja na uzembe.Ufisadi husababishwa na mambo kama vile tamaa inayowasukuma viongozi kunyakuwa mali ya umma kiharamu kwa manufaa yao binafsi bila kuwajali wengine. Hili limesababisha unyakuzi wa mashamba makubwa makubwa ya umma na walio katika mamlaka licha ya kuwa bado kungali na maskwota ambao hawana hata mahali pa kulala. Mali ya umma kama vile viwanja vya shule pia vimechukuliwa kupitia kwa njia zisizokuwa za haki. Wanaotekeleza haya wanazidi kunufaika kupitia kwa njia zisizokuwa za haki huku wananchi wa kawaida wakiendelea kuumia kutokana na athari za ufisadi.

Vyeo na nafasi za kazi vinakuwa vya wale ambao wana uhusiano wa kikabila au hata kisiasa na viongozi kwa hivyo wale ambao hawana watetezi, wanabaki wakihangaika ingawa wamehitimu katika nyanja mbalimbali. Ufisadi katika jamii hukuzwa na mambo kadha wa kadha. Were (1983) anasisitiza kwamba tofauti na mataifa mengine ulimwenguni, viongozi barani Afrika wamekuwa mstari wa mbele kupalilia ufisadi .Ingawa imekuwa ikishuhudiwa uundaji wa tume kadha wa kadha za kuchunguza ufisadi, baadhi ya matokeo ya tume hizi hayana manufaa yoyote au hayajulishwi kwa umma. Haya yanatokana na sheria dhaifu ambazo haziwapi wananchi mamlaka ya kuchukua hatua yoyote au kufuatilia matukio haya.

Iwapo jamii itakuwa na sheria kama hizi basi wanajamii hufanya watakalo kwa kuwa wao wana uhakika hakuna sheria yoyote itachukuliwa dhidi yao. Viongozi wa kisiasa huendeleza ufisadi wakifahamu kuwa sheria walizohusika kuzitunga ni dhaifu na kwa hivyo zinawapendelea. Katika hali ambapo viongozi wanapatikana kuhusika baadhi yao hujiuzuluili kuruhusu uchunguzi kufanywa ilhali wengine wanakatalia katika nafasi zao.

Vikaragosi au vibaraka hutumiwa na viongozi kuendeleza ufisadi. Hawa ni watu ambao licha ya kuwa na utawala mbaya wao hawaoni hitilafu yoyote ila kazi yao huwa ni kuwasifu viongozi na kuendelea kusifia hata yale ambayo hayafai. Katika kufanya hivyo wananchi wanashawishika kuwa viongozi hawa ni waadilifu na wanastahili kuendelea kuongoza. Nchi inapokuwa na watu wa aina hii inakuwa vigumu kumaliza ufisadi na badala yake ufisadi unapaliliwa.

Ufisadi huwa na athari nyingi katika nchi husika na wanaoathirika ni wananchi. Ufisadi hupelekea kuzorota kwa nchi kutokana na matumizi mabaya ya fedha. Wananchi kwa upande mwingine wanaishi maisha ya dhiki kwa kuwa inakuwa vigumu kukidhi mahitaji yao. Kuzorota kwa uchumi husababisha kuongezeka kwa bei hata ya vyakula na huduma zingine za umma kwa hivyo umasikini husakini na kukita mizizi miongoni mwa wananchi.

Ufisadi pia husababisha kukwama kwa miradi ya kiserikali na huduma nyinginezo baada ya miundo msingi kama vile shule na barabara kusahaulika au kutotiliwa maanani.Haya yanasababisha nchi kutokuwa na maendeleo. Hatimaye haya huigawanya jamii ambayo inakuwa na matabaka mawili huku wachache wakifaidika ilhali wengine wanazidi kuumia.Nyingi ya nchi ambazo viongozi wanaendeleza uongozi mbaya huongoza nchi kwa kimabavu kupitia kwa wasemi wachache katika serikali.

Katika nchi ambazo viongozi wanaendeleza uongozi mbaya, baadhi ya watu hasa walio katika uongozi, hawafuati sheria za nchi. Wao hutenda yanayowanufaisha na kupuuza sheria. Hata baada ya kukiuka sheria viongozi hawa hawachukuliwi hatua yoyote kwa hivyo nchi inakuwa ni ya wachache. Uongozi mbaya unadhihirika pale tunapokumbana na kudorora kwa huduma za umma ambazo zinasimamiwa na viongozi waovu. Hizi ni kama ukosefu wa dawa au matibabu ya kuridhisha zahanatini, mfumo duni wa elimu, uchafu wa mazingira, ukosefu na uchafuzi wa maji.

Hata hivyo wananchi wanaokandamizwa kwa njia ya aina hii wanabaki hawana lingine ila kupigania haki zao na kuleta ukombozi wa jamii husika. Miaka ya baada ya uhuru imekuwa na waandishi ambao wameangazia suala hili la uongozi mbaya ambao unaendelezwa katika nyingi ya nchi za hapa barani Afrika.

### 2.3.2.2 Utabaka

Muriithi (2013) anaeleza utabaka kama hali ya jamii kugawika katika makundi kadhaa kulingana na uwezo wao wa kiuchumi. Katika hali kama hii, wachache ndio wanaomiliki rasilimali. Mara nyingi mfumo wa kibepari hupelekea kuwepo kwa utabaka. Sarara (1997) akimnukuu Ngara (1985) anaendelea kusema kuwa jamii yenye matabaka, nguvu za kiuchumi huwa na watawala ambao wanahodhi nyenzo za uzalishaji mali na kwamba tabaka hili la juu ndilo husimamia elimu na itikadi katika jamii.Wachochole ambao ndio wa tabaka la chini huendelea kuumia na hata kuuza nguvu zao kwa wale wa tabaka la juu.

Utabaka umekuwepo tangu enzi za wakoloni ambapo wazungu walikuwa wa tabaka la juu ilhali waafrika walikuwa ndio wa tabaka la chini. Hali hii ilidhihirishwa na kuwepo kwa maeneo ya makaazi ya wazungu ambayo yalikuwa ya kifahari huku waafrika wakiwa wametengewa maeneo yao. Waafrika hawa walikuwa wanawatumikia tabaka la juu kwa mishahara duni.

Kazi za kifasihi ambazo zimeshughulikia suala hili la utabaka ni kama vile kazi ya Hussein (1971) ambapo kuna matabaka mawili makuu yanayowakilishwa na Kitaru na Juma. Familia ya Juma inawakilisha tabaka lililorithi kutoka kwa wazazi ilihali lile la Kitaru linawakilisha ni lile lilipokea elimu ya kizungu na ndilo lilishika hatamu ya uongozi baada ya uhuru. Hali hii pia inadhihirishwa na kuwepo kwa maeneo ya kifahari ambayo yanamilikiwa na wahusika wachache wa tabaka la juu huku wale wengi wa tabaka la chini wakipatikana katika mazingira duni yaliyosheheni ukata.

Mgawanyiko huu ni wa kiuhalisia katika mataifa mengi hapa Afrika ambayo yanatawaliwa na uongozi mbaya. Baada ya kuondolewa kwa mkoloni, waafrika walioshika hatamu ya uongozi waliongozwa na tamaa na ubinafsi katika kujinyakulia mali. Hali hii ilisababisha waafrika wachache waliomiliki rasilimali kujitengea sehemu zao za makaazi. Aghalabu kundi hili linawakilisha matajiri huku wenzao wa tabaka la chini wakiishi maeneo yao ya kimasikini.

Kazi za fasihi ya Kiswahili zimeshughulikia suala hili kwa kubainisha matabaka haya mawili kupitia kwa wahusika wao.Walibora (2012) anadhihirisha haya kupitia kwa Imani na Amani ambao walikuwa wa tabaka la chini na waliishi mitaa ya wachochole

kama vile Ulitima. Nasaba Bora kwa upande mwingine aliishi mitaa ya kifahari kwani alikuwa ni tabaka la juu. Sawa na hali ilivyokuwa katika utawala wa wakoloni, watoto wa wale wa tabaka ya juu wanasomea shule za kifahari na hata matibabu ni katika huduma za afya ambazo vilevile ni za kifahari na ambazo mtu wa tabaka la chini hawezi kumudu.

Wanaowakilisha tabaka la chini hupatikana wakijaribu kujikwamua kwa kufanya kazi za sulubu na hata kuwatumikia wale wa tabaka la juu. Wale wa tabaka la chini hujipata wakijishughulisha na maovu ya aina mbalimbali ili waweze kujikimu kimaisha. Tabaka hili la chini huwakilishwa na wasio na elimu pamoja na wale wanaopatikana katika vibanda

#### 2.3.2.3 Ukosefu wa haki

Katiba ya Kenya (2010) inatambua nyingi ya haki za kibinadamu kama vile haki ya kuishi, haki ya usawa wa kibinadamu bila kubaguliwa, haki ya kuwa huru na kuhakikishiwa usalama, haki ya kuabudu miongoni mwa haki nyinginezo.Lisilo haki hufanywa kuwa haki kulingana na anayetenda au anayetendewa. Wananchi hukumbwa na dhuluma wasipate haki zao.Baadhi ya vitendo vinavyoonyesha ukosefu wa haki ni kama vile watu kufungwa jela bila ya hatia au hata kupatiwa nafasi ya kujitetea. Wananchi pia hunyimwa haki zao wakati viongozi wananyakua mali ya wanyonge na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kwa kuwa wao ndio walio katika mamlaka. Hatimaye wanyonge wanabaki wakitaabika na kubaki bila hata makao.

Katika mataifa ya aina hii, watoto pia hunyimwa haki zao kwa kutumiwa na viongozi kwa manufaa yao. Licha ya kuwa si haki kwa mtu kumwajiri mtoto wa chini ya umri wa miaka kumi na minane, mabwenyenye huvunja sheria hii kila uchao kwa kuwaajiri watoto wadogo na kuwalipa mishahara duni kama inavyoshuhudiwa katika Walibora(2012) ambapo mabwenyenye kama Bwana Maozi wanawaajiri vijana wachanga kama D.J ambaye alikuwa hajamaliza hata masomo ya shule ya msingi.

Ukosefu wa haki katika uongozi fulani ndio chanzo cha maonevu na hata dhuluma za aina mbali mbali dhidi ya watu ambao hawana uwezo wa kiuchumi. Tatizo hili litaweza kusuluhishwa iwapo tu patakuwepo na utetezi wa haki za kibinadamu na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa watu ambao wanavunja sheria.

#### 2.3.2.4 Umasikini

Hope (2004) anaeleza kwamba umasikini unaweza kuainishwa kutegemea vigezo tofauti tofauti kulingana na jamii husika. Umasikini kulingana nasi tutauchukulia kama hali ya kukosa mahitaji ya kimsingi katika maisha ya kila siku Hii ni pamoja na ukosefu wa lishe bora, makaazi na hata matibabu. Akirejelea taarifa ya benki la dunia kuhusu umasikini (2001) anasema ukadiriaji wa hivi karibuni unaonyesha kuwa takriban asilimia arobaini na saba ya waafrika katika mataifa yanayoendelea ni masikini huku wengi wao wakiwa katika Afrika Mashariki na Nigeria. Umasikini barani Afrika unahusishwa na uongozi mbaya baada ya Afrika kupata uhuru. Kiini kikubwa kikiwa ni ufisadi miongoni mwa viongozi hawa.

Ndegwa na Herbold (1984) wanasema mataifa mengi yanayoendelea barani Afrika yanakumbwa na changamoto ya mikopo kutoka mataifa ya magharibi. Mikopo hii inakuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya uchumi katika mataifa haya. Hali hii pia inasababisha mataifa haya kuwa na utawala unaoyumbayumba kutokana na ukweli kuwa mataifa ya kimagharibi yanakuwa na uwezo mwingi au nguvu nyingi za ushawishi huku yakijiegemeza kwa madeni yanayodaimataifa haya ya Afrika.

Nyamemba (2012) anahusisha umasikini na ongezeko la idadi ya watu nchini.Kulingana na sensa ya (1963), idadi ya watu ilikuwa million nane. Idadi hii imeongezeka hadi milioni 38.6 kulingana na tarakimu za sense ya 2013. Kwa hivyo ongezeko hili ambalo ni la kiwango cha juu sana limekuwa na athari kubwa kutokana na kuwa watu wanang'ang'ania nafasi chache za uzalishaji wa uchumi nchini.

Umasikini kwa hivyo ni suala la kiuchumi ambalo hupaliliwa na mfumo wa kisiasa ambao unaishia kuwanufaisha wachache. Katika bara la Afrika, umasikini una mizizi yake katika utawala wa wakoloni ambao walijinufaisha na rasilimali za Afrika. Ukosefu wa usawa katika ugavi wa rasilimali za kitaifa ukachangia pakubwa katika kuwepo kwa umasikini. Hili liliendelezwa na waafrika walioshika hatamu baada ya kuondoka kwa mkoloni kupitia kwa utawala mbaya na ubinafsi

Ukosefu wa ajira pia umechangia pakubwa katika ongezeko la umasikini. Tatizo hili limesababisha vijana kuhamia mataifa mengine kwa minajili ya kujikimu kimaisha. Katika hali kama hii, mataifa mengi ya ulaya yanaendelea kupata nguvu kazi na hivyo

kujiendeleza kiuchumi. Hata baada ya vijana hawa kupata ajira, wengi wanabakia ugaibuni kwa kuhofia hali ngumu ya kimaisha hapa Afrika.

Umasikini ni mojawapo wa masuala ambayo yamekuwa yakiangaziwa katika kazi nyingi za kifasihi na kwa hivyo kuzua hali ya kutokuwa na usawa katika jamii. Katika hali kama hii, kuna haja ya kuwepo na ukombozi ambapo wananchi watakuwa na nafasi ya kugawana rasilimali kwa njia isiyo ya ubinafsi.

### 2.3.3 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulika na baadhi ya vichocheo katika jamii ambavyo huisukuma jamii kutaka kujinasua katika changamoto au matatizo zinazopitia. Ni vichocheo kama vile ukosefu wa haki, umasikini, ufisadi, ukoloni mamboleo, utabaka na hata uongozi mbaya ambavyo vimetuwekea msingi wa kuchanganua kuhusu aina mbalimbali za ukombozi katika kazi tulizoteua. Vijana wanapokumbana na changamoto hizi katika maisha yao wanapata msukumo wa kutafuta suluhu la kudumu kwa jamii nzima

## SURA YA TATU

## MCHANGO WA VIJANA WA KULETA UKOMBOZI KATIKA KAZI ZA LEONARD SANJA

### 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili tulishughulikia changamoto mbali mbali ambazo hukumba jamii. Tulibainisha kuwa hali hizi si za kuridhisha na kwa hivyo vijana wakiwa miongoni mwa wanajamii katika kazi tulizoteuwa wanashirikiana pamoja ili kuinasua jamii kutoka kwa masumbuko haya.

Katika sura hii tutashughulikia mchango wa vijana katika kuleta ukombozi wa jamii katika hadithi fupi ya *Mwavyaji wa Roho*, *Zinguo la Mzuka* na katika *Yasinya*. Wanajamii katika kazi hizi wanakumbwa na changamoto anuwai na kuna haja ya kuangazia jinsi vijana wanachangia katika kuleta ukombozi kutokana na changamoto hizi. Kabla ya kuchunguza mchango wa vijana, tutaanza kwa kuandika muhtasari wa kazi hizi ili tupate taswira kamili ya hali za jamii katika kazi hizi.

#### 3.1.1 Muhtasari Wa "*Mwavyaji wa Roho*"

"Mwavyaji wa Roho" ni hadithi fupi katika Diwani ya*Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Hadithi inaanza kwa kuonyesha hatua za kisheria ambazo huchukuliwa viongozi waliostaafu katika mataifa ya ughaibuni kinyume na mataifa ya Afrika kama anavyoeleza Saida kuhusu jamii katika "*Mwavyaji wa Roho*". Viongozi wa Kiafrika wanatumia nafasi zao vibaya kwa kuwanyima kandarasi wale ambao hawashirikiani nao kuendeleza uongozi mbaya. Vijana wanaonekana wakizurura ovyo mitaani kwa kukosa ajira huku wakijiingiza katika maovu kama vile matumizi ya mihadarati na ukahaba.

Kitambi ambaye ni amiye Jael ni mtu ambaye anamiliki mali nyingi pale mjini. Ana sifa za kuwanyanyasa kimapenzi wasichana wachanga na hatimaye anawatelekeza baada ya kuwahadaa au kuwakaba.Vile vile anaendeleza biashara haramu ya mihadarati kwa ushirikiano na Jael ambaye ni mwanafunzi katika mojawapo wa vyuo kikuu pale mjini. Jael ndiye anayesambaza madawa ya kulevya kwa vijana na hata

wanafunzi wa shule za msingi. Wote hawa wanakusanyika chumbani mwa Jael kila mtu akiwa na hela mkononi tayari kuuziwa "unga" kama walivyorejelea madawa haya ya kulevya.Kitambi ana ushawishi mkubwa na kwa hivyo wakati magari madogo yalipigwa marufuku kuingia mjini, mamia ya mabasi yaliyomilikiwa na Kitambi yalitumika katika uchukuzi wa abiria mijini badala yake.

Jael na rafiki yake Saida wanaishi pamoja lakini wawili hawa wana tofauti kubwa kimaadili. Licha ya kuwa Saida alielewa vyema kuwa biashara hii haramu ilikuwa na mapato mazuri, anakataa katakata kujihusisha nayo. Anawaza iwapo kuna wakati ambapo nchi za bara la Afrika zitafikia kiwango cha kuwahukumu watu kama Kitambi na viongozi wengine wanaoendeleza maovu katika jamii.

Jael aliposhikwa na kuwekwa kizuizini kwa tuhuma za kuuza mihadarati, alimtuma Saida kwa amiye ili amfahamishe yaliyokuwa yamejiri. Afisini mawazo ya Kitambi ni kwamba Saida ni kati ya wasichana waliojileta kwake lakini kwa haraka Saida anampasha habari na kuondoka licha ya kushawishiwa kwamba angesindikizwa hadi chuo. Kijana huyu anajinasua asije akajihusisha nao kwa vyovyote vile. Hatimaye Jael aliachiliwa huru ilipobainika kuwa alikuwa mpwa wake Kitambi. Saida alizawadiwa nyumba ya kifahari katika mtaa wa wakwasi baada ya kuonywa asiseme lolote nao askari waliomkamata Jael wakapewa vitisho na kisha kupatiwa hongo.

Jael alijaribu kumshawishi Saida waungane kuendeleza biashara ile haramu lakini badala yake Saida alitatizwa na mawazo yake huku akiwaza kuhusu wazazi wanaolia kuhusu wana wao ambao wamepotea katika madawa ya kulevya. Aliwaza kuhusu vijana hawa ambao ndio msingi wa kizazi kijacho akaona huruma kubwa. Mawazo haya pamoja na maovu mengine ndiyo yalimsababisha Saida kurejesha funguo za nyumba aliyokuwa amepewa na kuwa mpinzani mkuu wa utawala wa Kitambi. Alihiari kuhamia vibandani walikoishi makabwela badala ya kuwa mfuasi wa Kitambi.

### 3.1.2 Muhtasari wa*Zinguo La Mzuka*

*Zinguo la Mzuka* ni tamthilia ambayo inashughulikia masuala kama vile athari za ukoloni katika mataifa ya bara la Afrika, ukoloni mamboleo na uongozi mbaya katika mataifa haya baada ya kupata uhuru**.** Katika onyesho la kwanza mwandishi

anazungumzia kuhusu ukoloni ulioendelezwa na “Mweupe” Katika Afrika ambapo wakoloni walijinyakulia raslimali na mapato mengine na kuifilisisha Afrika. Licha ya kuwa “Mweusi” au mwafrika alifikiria kuwa mkoloni alikuwa amefukuzwa bado mkoloni alikuwa akiendeleza utawala wake kwa Waafrika na alikuwa na ushawishi mkubwa kama hapo awali. Wananchi wa Kusinyikahawakuchukua hatua yoyote wakati nchi yao ilikuwa inafilisiwa ila kulalamika tu. Baada ya Mzuka kunyakua mali ya Kusinyika, Zinguo alijaribu kumfukuza lakini mbinu alizotumia hazikufua dafu. Mzuka aliwakejeli waafrika akisema hawakuwa na elimu ya kiteknolojia au uwezo wa kujitawala. Baadaye Zinguo alishirikiana na Mzuka katika kujinyakulia mali ya Kusinyika na kuwanyanyasa wananchi. Sichana mfanyakazi wake Zinguo ni kijana ambaye amepevuka kimawazo tofauti na vijakazi wenzake ambao wanakandamizwa na waajiri wao. Anapitia dhuluma za kimapenzi anapokuwa nyumbani kwa Zinguo. Anapigania haki za wafanyikazi na hata wananchi ambao walikuwa wakinyanyaswa. Anaililia bara ya Afrika anaposema kuwa imefilisiwa na kuachwa uchi. Hatimaye wanakusinyika walizinduka na hapo ndipo vijana walionyesha mchango mkubwa wa kupigania ukombozi dhidi ya uongozi mbaya. Waliungana na Polisi na Dira hadi wakafanikiwa kuwatia ndani Zinguo na rafiki yake Kaza. Baada ya Zinguo kung’olewa mamlakani serikali mpya na iliyohuru ilichukua uongozi na kuwahusisha hadi vijana ambao walikuwa wamesahaulika katika uongozi wa Zinguo.

### 3.1.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Yasinya*

*Yasinya* ni riwaya ambayo inahusu wanajamii ambao wamegawika katika makundi au matabaka mawili. Tabaka la juu linawakilishwa na Kifuja, Chebaskwony, Dkt Balaa, Mayowe pamoja na Angusha. Kundi hili ndilo linatawala Wanakusinyika likiongozwa na Kifuja. Tabaka hili linaishi katika maeneo ya kifahari kama vile mtaa wa Bwenyenye. Sehemu hii ilijitenga na maeneo mengine ya Mabonde ambako kuliishi watu wa tabaka la chini.

Tabaka la chini linawakilishwa na Asisi, Kijasiri, Kipokeo, Aisha, Emali na Sifichi. Asisi ni kijana ambaye amemaliza masomo na kupata shahada. Yeye ndiye anayeongoza kundi hili katika kupigania haki zao. Makazi ya kundi hili ni duni. Kwa mfano hali ya mabanda ya Kambisuswa yalikuwa ya kutisha. Mlikuwa na maji machafu ambayo aghalabu yalichanganywa na majitaka yaliyotokana na mabomba

yaliyokuwa yanavuja. Maji yale pia yalinywewa. Huduma muhimu kama vile hospitali zilikuwa muhali kupatikana katika eneo hili. Wakaazi waliishi katika mabanda yaliyokuwa yameinamiana licha ya kuwa na viongozi waliokuwa wamewachagua kuwawakilisha.

Kifuja na wenzake walikuwa wamejinyakulia mashamba makubwa makubwa na wao ndio walioendeleza biashara zilizokuwa na mapato ya juu bila kuwapa wengine nafasi. Wana wake walikuwa wanasomea shule za kifahari na baadhi yao walikuwa tayari wamepata ajira. Ingawa watu kama Asisi na Kijasiri walikuwa wamehitimu na kupata shahada, wao hawakupata mwanya wa kupata ajira yoyote kutokana na kuwa wao walikuwa wana wa walalahoi. Hata hivyo wanajitahidi kwa kufanya kazi duni ili waweze kukimu mahitaji yao ya kila siku pamoja na kuhakikisha kwamba wanapigania nafasi zao.

Maovu mengi katika eneo la Mabonde yanaendelezwa na waliokuwa katika mamlaka yaani akina Kifuja. Wao ndio wadhamini wakubwa wa ulanguzi wa madawa ya kulevya yanayouziwa wanafunzi wa shule za msingi na vyuo vikuu. Huni ambaye ni mjukuu wa Kifuja alikuwa ametajirika kutokana na uuzaji wa madawa haya ya kulevya. Kifuja alikuwa na ushawishi mkubwa kwa mkuu wa polisi ambaye alikuwa anakabiliana na ulanguzi wa madawa ya kulevya. Mayowe naye aliwatumia wanafunzi wa shule za msingi kumsaidia kuuza madawa haya kwa wenzao. Baada ya mzazi fulani wa  mabondeni kulalamika, alinyamazishwa kwa kupatiwa kiasi fulani cha pesa.

Mauaji ni uovu mwingine ambao uliendelezwa na viongozi hawa. Yeyote ambaye alionekana kuupinga uongozi wa Kifuja hatima yake ilikuwa kaburi. Mhadhiri wake Asisi aliuawa na hatimaye yeye Asisi akasingiziwa. Isitoshe Gwiji mhariri mkuu naye pia aliuawa kwa njia ambayo haikueleweka. Ilisubiriwa sheria ichukuliwe na haki itendeke lakini hili halikutimia. Kesi zilijaa kortini huku washukiwa wengi wakiwekwa ndani bila ushahidi wowote na pengine kuhukumiwa bila ya haki kutendeka.

Asisi aliwaongoza vijana wengine na wakaanzisha shirika la kupigania haki za watoto . Liwazo na Anao walikuwa wana wa mabwenyenye ambao waliungana na akina

Asisi na Kijasiri kuupinga uongozi dhalimu wa viongozi kama Kifuja na Mayowe. Vijana hawa waliwahamasisha vijana wengine kuhusu madhara ya madawa ya kulevya na hata haja ya kujikomboa kutoka kwa hali mbaya walizokuwa wakipitia. Kipokeo ambaye alikuwa amejiingiza katika uasherati hatimaye alibadilika na kuwa mwema baada ya kupatana na Asisi aliyempa wasia. Kijasiri pia aliwashirikisha wanamabonde wote ili kuhakikisha usawa wa jinsia zote  kuboresha maisha yao

Katika harakati za vita vya ukombozi vijana hawa walipata changamoto anuwai kama vile kufungwa jela kwa masingizio kama alivyofanyiwa Kijasiri alipojaribu kufanya uchunguzi kuhusu biashara haramu ya madawa ya kulevya iliyokuwa ikiendelezwa na Kifuja pamoja na Mayowe.  Licha ya dhuluma hizi vijana hawa walizidi kujitahidi kupigania haki zao na za Wanamabonde. Hatimaye juhudi zao zilizaa matunda baada ya kifo cha Mayowe na kutoweka kwa Kifuja baada yake kuona mambo yalikuwa yameharibika.

Kazi hizi zilibainika kuwa na maudhui mengi yanayolingana na vilevile yana wahusika vijana ambao wanachangia katika kukomboa jamii zao. Jamii katika kazi hizi zinashuhudia maovu kutoka kwa walio na nguvu za kiuchumi kama vile mzee Kitambi, Zinguo, Mweusi, Kifuja, Chebaskwoni na Angusha.Lukacs (1963) anaeleza uhalisia sharti ujihusishe na mambo halisi yanayotokea katika mazingira halisi kupitia kwa wahusika. Mihimili wa kwanza unasisitiza kuwa wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya binadamu wa kawaida. Hii ina maana kuwa wahusika katika fasihi huakisiyale yanayofanyika katika ulimwengu halisi. Wahusika vijana katika kazi hizi vilevile wanawakilisha vijana katika ulimwengu halisi. Wengi wao wanapatikana katika mazingira ya elimu na hata mitaani kama tunavyoshuhudia katika maisha ya kila siku. Vijana wakiwemo wale wa vyuo vikuu wameonekana wakijiingiza katika ulingo wa siasa na kujaribu kuwapinga viongozi ambao ni wa umri wa makamu.Baadhi yao wamefaulu kuteuliwa na wananchi kuwawakilisha katika bunge wakiwa na umri wa chini ya miaka thelathini na mitano.

Jamii katika *Zinguo la Mzuka* inakumbwa na matatizo kama vile, ukoloni mamboleo, umasikini na hata ukosefu wa elimu bora. Mhusika Sichana na vijana wengine katika

jamii ya wanakusinyika wanaungana kupigania uhuru wa jamii zao. Wimbo aliouimba Sichana walikuwa wakiuimba shuleni Kusinyika kudhihirisha kilio cha haki kupitia kwa kizazi kichanga. Ni kupitia wimbo huu ambapo mwandishi anaonyesha matumaini ya kubadilika kwa hali mbaya ya wanakusinyika wakiongozwa na vijana katika siku za usoni. Matatizo yanayokumba jamii hii si tofauti na yale yanayokumba jamii katika ulimwengu halisi. Sichana anawakilisha vijana waliokosa elimu katika jamii zetu kutokana na ufukara. Licha ya kuwa viongozi wengi ni wazee, hali inaonekana ikibadilika na vijana sasa wameanza kupata nafasi ya kutetea haki zao na za jamii zao.

Wahusika vijana katika *Yasinya* wanadhihirisha mchango wao mkubwa katika juhudi zao za kupigana na maovu yanayoendelezwa na viongozi waovu kama vile Kifuja na Mayowe. Wanamabonde wanapopigania uhuru wao na kuunyakua kutoka kwa wakoloni, wanawaamini viongozi waafrika kwamba wangeleta mabadiliko makubwa na ya kuwafaa baada ya utawala wa mkoloni. Mambo hayakuwa kama walivyotarajia na badala yake viongozi hawa waliungana pamoja kujinyakulia mali ya umma, kuendeleza ufisadi na kutekeleza maovu mengine ambayo yaliwapa vijana kama Asisi, Anao, Kijasiri, Kipokeo na wengine ari ya kuiwakilisha jamii yao ili waikomboe kutokana na maovu ya viongozi hawa. Haya ni matukio ambayo yanaweza kudhihirika katika ulimwengu halisi hasa katika nchi za Afrika. Viongozi wengi ni miongoni mwa wale ambao walikuwepo katika utawala wa wakoloni. Badala ya kuwajibika na kuwanufaisha wananchi, viongozi hawa huongozwa na tamaa na ubinafsi wa kujinufaisha. Vijana wakiongozwa na Asisi katika kazi hii wanapatikana katika vyuo vikuu na wengine hawajachukua muda mrefu kutoka walipohitimu masomo ya chuo kikuu. Vijana kama hawa wanashuhudiwa kila uchao wakiandamana na kutetea haki zao hasa pale vyuoni.

Katika *Mwavyaji wa Roho* Kitambi anaendeleza ulanguzi wa madawa ya kulevya na kuwaharibu vijana wa shule za upili na chuo kikuu. Anamhusisha Jael mpwaye ambaye ni mwanafaunzi wa chuo kikuu na uuzaji wa mihadarati ili kujinufaisha yeye mwenyewe huku akiangamiza jamii. Jamii vile vile inashuhudia maovu mengine ambayo yanalemaza maendeleo yao na hata kusababisha dhiki na masumbuko. Hata hivyo, mwandishi amewapa vijana nafasi kubwa na kuonyesha mchango wao katika

kuleta ukombozi kupitia kwa mhusika Saida ambaye ni kijana wa chuo kikuu. Saida amedhihirisha mchango wake mkubwa wa kupigana na maovu ya viongozi dhalimu na wenye ubinafsi mkubwa. Mazingira katika kazi hii ni ya kihalisia kwa kuwa yanawakilisha yale ya vyuo vikuu katika ulimwengu halisi ambapo wanafunzi vijana wanaishi kwenye vyumba vyao na kuendeleza shughuli zao za kila siku. Maovu ya ulanguzi wa madawa ya kulevya yamekuwa yakiangaziwa na vyombo vya habari na wakati mwingine huhusishwa na viongozi.

Katika sehemu hii tutachunguza na kuchanganua kwa pamoja mchango wa vijana katika kuleta aina mbalimbali za ukombozi katika kazi hizi tatu ili tuweze kuwa na picha kamili ya jinsi mwandishi huyu amewapa wahusika vijana nafasi hii muhimu ya ukombozi katika jamii zao. Hali mbalimbali za kiukombozi ambazo tutazichanganua kwa pamoja ni: Umasikini, Madawa ya kulevya, Unyanyasaji kwa wanawake na Ufisadi.

### 3.2.1Ukombozi dhidi ya umaskini

Wamitila (2002) anaelezea kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wa kazi za kihalisia hutoa picha ya wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika.

Umasikini ni suala  ambalo limeangaziwa na mwandishi katika kazi hizi. Ametuchorea picha ya wanajamii ambao wanawakilisha baadhi ya wananchi katika nchi yetu. Hali ya ufukara ya wahusika katika kazi hizi ni kioo cha jamii halisi kwa kuwa hali yao ni ile tunayoshuhudia katika maisha ya kila siku. Maudhui haya yamekuzwa  kupitia kwa kijakazi wake  Zinguo ambaye ni Sichana katika *Zinguo la Mzuka*. Kupitia kwa mhusika huyu ni wazi kuwa jamii ya kijana huyu inamtegemea yeye kwa mahitaji yao yote. Wimbo wake unadhihirisha mtu ambaye anafadhaika kutokana na hali ya familia yake ya uchochole. Anaimba na kusema

Lakini
Huduma nalipwa
Maslahi Napata
Nitasoma na nini?
Najistiri kwa matawi
Nyumba ya mama ganjo
Naliwa na funza sijafa?
Viatu ni ghali Sichana.
Ukinunua viatu mama na
Ndugu zako watazongwa
na njaa.... (uk 26)

Katika wimbo huu wa Sichana inabainika kwamba wanakusinyika wana uchochole uliokita mizizi kiasi kwamba wanawatafutia ajira wanao wakiwa bado wachanga ili waweze kuwasaidia kulea watoto.Vijana kama Sichana wanalazimika kufanyishwa kazi ngumu na hata kudhulumiwa na waajiri wao ili wapate kipato cha kusaidia familia zao. Ni wazi kwamba wazazi wake Sichana wanaishi katika mabanda huku hali yao ikiwa ni ya kusikitisha.Umasikini ndio chanzo cha ukosefu wa elimu kwa vijana katika nchi ya Kusinyika jambo ambalo linamhuzunisha Sichana na kwa hivyo kulilia ukombozi wake. Licha ya haya Sichana anafanya kazi kwa bidii ilmradi wazazi wake na ndugu zake wapate angalau vyakula na mavazi.Hata baada ya kulipwa mshahara wa mwisho wa mwezi Sichana anahiari kutonunua viatu ili awatumie wazazi wake pesa hizo.

Umasikini katika *Yasinya* ulikuwa umekithiri katika eneo la Mabonde kutokana na uongozi mbaya wa bwana Kifuja na wenzake. Wananchi walikumbwa na magonjwa kutokana na unywaji wa maji machafu na mazingira mabovu. Mazingira katika eneo hili yanawakilisha baadhi ya vitongoji katika ulimwengu halisi hapa nchini ambapo hali hairidhishi hata kidogo. Kutokana na umasikini huu, vijana walionyesha mchango wao katika kumsaidia ajuza aliyekuwa mgonjwa. Alilazimika abebwe kwa pikipiki kutokana na ukosefu wa hela za kukomboa gari la kumpeleka hospitalini. Mwandishi amewapa vijana nafasi muhimu ya kuikomboa jamii kutokana na hali hii kupitia kwa Asisi, Kijasiri na Liwazo. Vijana hawa walikuwa wameelimika wakilinganishwa na vijana wengine. Walitumia elimu yao na hela zao ili kuwanusuru wananchi ambao waliokuwa wameemewa na maisha.

Mchango wao unadhihirika wanaposhirikiana kutafuta gari lililompeleka ajuza hospitali ya wilaya. Liwazo aliahidi kugharamia matibabu ya mgonjwa huyu hadi pale atakapopata afueni. Wanawake waliokuwa wameandamana na ajuza huyu walimshukuru Liwazo kwa msaada wake kwa kuwa hakuna aliyekuwa na uwezo wa kifedha. Asisi naye alichangia kwa kumlipa mwendeshaji wa pikipiki ambaye hakuwa na matumaini ya kupata chochote kutokana na uchochole wa wateja wake. Mwendeshaji pikipiki vilevile alikuwa miongoni mwa Wanamabonde waliokuwa katika harakati za kujikomboa kutokana na hali yao duni ya kimaisha.Wanawake waliokuwa wamempeleka mgonjwa hospitali walibahatika kulipiwa pikipiki ili iwarejeshe manyumbani kwao.

Vijana wa Mabonde wamekulia katika mazingira ya uchochole kiasi cha kwamba hata karo ya kujiunga na chuo kikuu haikupatikana.Wale wanaobahatika kujiunga na chuo kikuu kama vile Asisi, Kipokeo na vijana wengine wanakumbwa na changamoto hii ya kukosa karo. Hata hivyo vijana hawa wanajitahidi kutafuta vibarua ili waweze kupata karo na mahitaji mengine. Kwa kufanya hivi vijana hawa wanapigana kujikomboa kutoka kwa ufukara ili wakimaliza masomo yao wawe watu wa kujitegemea na kutegemewa na jamii. Mwandishi anatufahamisha kuwa “Asisi alifanya vibarua akajilipia karo katika chuo kikuu cha kitaifaambako alikuwa akimalizia shahada yake ya uanasheria....”(uk10).

Wananchi katika eneo la Wamakonde waliishi maisha ya ufukara kiasi cha kukosa makaazi mema na afya bora. Haya yote yalisababishwa na ubinafsi pamoja na tamaa ya viongozi wao. Vijana kama vile Asisi, Kijasiri na Anao waliungana na kuunda shirika ambalo lilikuwa likipigania afya na makaazi bora kwa wananchi wote. Anao alipinga vikali maonevu yoyote licha ya kuwa alikuwa mwana wa mmoja kati ya viongozi ambao waliendeleza dhuluma kwa wananchi. Tunaelezwa yafuatayo kuhusu kijana huyu:

> ....si haba alichangia mradi wa akina Asisi na Kijasiri
> Uliopiganiaafya na makaazi bora. Alisaidia kuchimba
> vyoo, kuwapa wakaazimabati na kuwashirikisha vijana
> katika shughuli mbali mbali za maendeleo. (uk82).

Katika kufanya hivi vijana hawa waliboresha maisha ya wakaazi wa Mabonde na kubadilisha sura ya eneo hili ambalo lilikuwa halikaliki hapo awali. Vijana waliokuwa hawana matumaini kutokana na ukosefu wa ajira sasa walihusishwa katika ujenzi wa nchi yao. Anao vilevile aliendesha shirika ambalo lilipigana na madawa ya kulevya hasa miongoni mwa vijana ambao walikuwa wamehangaika kutokana na ukosefu wa ajira. Juhudi hizi ziliwasaidia waliokuwa wamejiingiza katika madawa haya kurekebisha mienendo yao ili hatimaye waweze kuyakimu maisha yao.Ni wazi kuwa wanamabonde walikuwa wanaishi maisha ya uchochole na yasiyo na matumaini chini ya uongozi wa Kifuja na wenzake. Asisi na wenzake wanatoa mchango mkubwa kwa wakaazi hawa na kuwaahidi matumaini ya maisha bora ya usoni.

Baadhi ya vijana katika vyuo vikuu hujipata wakijiingiza katika ulanguzi wa madawa ya kulevya ili waweze kujikimu kutokana na hali yao ya kimasikini. Wengine ni kutokana na changamoto za ukosefu wa ajira. Katika hadithi ya *Mwavyaji wa Roho* wengi wa wahusika vijana wanajiingiza katika anasa mbalimbali na hata ulanguzi wa madawa ya kulevya. Vijana wameathirika na madawa haya kiasi kwamba hawawezi kuacha kuyatumia. Kupitia kwa mhusika Saida mwandishi amedhihirisha kuwa vijana wana uwezo wa kujikomboa kutoka kwa tabia kama hizi hata kama wametoka katika familia ambazo hazijiwezi kiuchumi.

Licha ya kuwa Saida ni mwanafunzi ambaye ametoka katika familia isiyojiweza kiuchumi na ni rafiki yake Jael ambaye wanaishi katika bweni moja kwenye chuo kikuu, yeye hajihusishi na biashara haramu ya kutumia madawa ya kulevya. Inabainika kwamba Jael anashirikiana na ami yake Kitambi katika kuwauzia vijana madawa haya. Saida anapata nafasi ya kukutana na Kitambi wakati Jael alikuwa ametiwa kizuizini. Kwa kuwa Saida alikuwa kijana mwenye maadili aliweza kujinasua licha ya kushawishiwa na wawili hawa. Hii ilikuwa ni baada yake kujua kuwa Kitambi alikuwa akihusika na uuzaji wa madawa ya kulevya. Alipotumwa na Jael kumfahamisha Kitambi kuwa alikuwa amewekwa kizuizini. Saida alikumbuka visa alivyokuwa amevisikia kuhusu mihadarati na kwa hivyo akaamua kutojihusisha kabisa.

Vijana wa jinsia zote walifika pale bwenini kununua madawa ya kulevya na baadhi yao waliyatumia wakiwa mle chumbani. Saida anaonekana akisumbuka kimawazo na kuwashutumu wale waliokuwa wanawauzia vijana madawa haya. Jael anamuahidi kwamba angeongea na Kitambi ami yake ili naye Saida apate pesa kupitia kwa njia hii hata hivyo badala ya Saida kukubaliana na Jael, Saida anajipata katika lindi la mawazo kuhusu vijana waliokuwa njiani kuangami kama inavyodhihirika hapa:

> Chumo dada, unadhani hawa wakubwa wanatoa wapi pesa zao?
> ..naweza kuongea naye kwa niaba yako ukitaka.
> Badala ya jibu, sura za wale vijana kwenye runinga zilinijia
> kwa kishindo....wazazi wao walikuwa wakilia na kuomboleza
> wakijiuliza walikuwa wamekosea wapi. ( uk 79)

Kupitia kwa mawazo ya Saida, sauti ya kilio cha ukombozi kutoka kwa wazazi na jamii kinasikika kikilia ukombozi wa vijana wanaojiingiza katika utumiaji wa madawa ya kulevya. Sauti hii pia inalilia sheria kuchukuliwa dhidi ya viongozi ambao wanajihusisha na ulanguzi wa madawa ya kulevya lakini hawachukuliwi hatua yoyote miaka nenda rudi. Wazazi wanasikika wakiomboleza hali ya wana wao na kusema,

> Tumezaa wana wetu na kuwalea vyema , sasa nyinyi na biashara yenu
> muwafanye vizuu! Mimi nafa jamani! Hakuna wa kuwadhibiti hawa
> papa na nyangumi? Uuuuiii ! mama alilia. (uk. 79)

Kilio hiki kinadhihirisha wazi kuwa vijana wengi wanatumia mihadarati huku ikibainika kuwa viongozi walikuwa wanahusika kwa njia moja.Kuwepo kwa kijana kama Saida katika jamii kama hii ilikuwa njia ya mwandishi kuonyesha kwamba vijana pia wana uwezo wa kuwa huru kutokana na upotovu wa aina hii.

### 3.2.2 Dhuluma kwa wanawake

Wellek (1960) anaeleza uhalisia kama uwasilishaji wa hali halisi ya maisha ya jamii kama yalivyo katika kipindi fulani cha wakati. Kulingana na haya mwanamke amechorwa kama mhusika ambaye anabadilika kiwakati. Wahusika wanawake wanaungana kupigania haki zao na hata za jamii kama ilivyo katika jamii husika. Dhuluma kwa wanawake ni tatizo ambalo limekuwepo tangu zamani hadi sasa. Wanawake wengi katika hali halisi wameshuhudiwa wakidhulumiwa na wanaume licha ya kuwa na sheria zinazomlinda kila mwananchi.

Mwandishi wa kazi hizi ameonyesha kwamba licha ya kuwa wanawake wengi wamepiga hatua kubwa katika maendeleo nchini, bado kuna baadhi yao ambao wanaendelea kudhulumiwa na jinsia ya kiume. Inabainika wazi kuwa wahusika wa jinsia ya kiume wanajiona bora kuliko wanawake au wanatumia nafasi walizonazo katika mamlaka ili waendeleze dhuluma kwa mwanamke. Haya yanajitokeza kupitia kwa Sichana, Kijasiri, Kipokeo na Sifichi. Hata hivyo wanawake hawa wanaonyesha juhudi zao za kujikomboa kutokana na dhuluma hizi.

Katika *Yasiny*a baadhi ya wanawake wanapitia dhuluma mbalimbali katika ndoa na kazini. Dhuluma hizi zinaendelezwa na wanaume ambao wanajiona bora au kuwaona wanawake kuwa dhaifu.Mazungumzo baina ya Kipokeo na Asisi yalibainisha kuwa Kipokeo alikuwa ametoka kwao nyumbani akiwa na umri wa miaka kumi na minne. Lakini alipofika mjini alikumbwa na dhuluma kama anavyoeleza

> .....Bosi alinikombolea nyumba ili niwe kipusa chake
> lakini nikagundua alikuwa na wasichana wengine....
> nikafunganya virago hadi hapa unaponiona...(uk 22)

Dhuluma kama hii inalenga kuishusha hadhi ya mwanamke na kumwona kama kiumbe dhaifu ambacho hakina uwezo wa kujimudu au kujitegemea. Licha ya kuwa Kipokeo alikuwa msichana mchanga alichukua uamuzi wa kupigania haki zake kwa kuondoka kule na kutafuta ajira kwingine kudhihirisha kwamba hata wasio na uwezo mkubwa wa kiuchumi wanaweza kujinasua kutoka kwa unyanyasaji wanaopitia. Ami yake Kipokeo vile vile alidhamiria kumuoza kwa mwanamume mmoja pale kijijini kwao akiwa bado mchanga. Mwanamume huyu alikuwa amempa ami yake Kipokeo magunia ya nafaka ambayo yangeuzwa ili kumlipia karo mtoto wa kiume wa ami.Kumwoza Kipokeo ndiyo malipo ambayo yalitazamiwa. Kipokeo alifaulu kujinasua kutokana na dhuluma hii alipoamua kutorokea mjini kutafuta ajira.

Kijasiri ni mfano wa vijana ambao ni thabiti katika kupigania haki za wanawake. Anapokuwa njiani anakutana na wanaume ambao wanamkosea heshima kama ilivyokuwa kawaida yao. Kijasiri kwa ujasiri aliwafokea wanaume wale na kudhihirisha haja ya kuwaheshimu wanawake na kuwaonea fahari kama binabamu wengine.Huyu ni kijana ambaye alikuwa ana maadili na heshima zake na hangestahimili kufanyiwa mzaha na wanaume ambao waliwaona wanawake kama

vyombo vya kujifurahisha kimapenzi.Kijasiri alisimama na kuwakazia macho na kusema“wanawake siyo mikokoteni wala matambara ama jaa ya kutupwa taka.Ni watu na watu wanastahili heshima. “Wana hadhi yao.” (uk 40)

Dhuluma kwa wanawake huwepo wakati mwingine kutokana na hali ngumu ambayo wanawake wanapitia katika maisha. Kwa mfano iwapo mwanamke ana changamoto fulani na ambayo suluhisho litapatikana kutoka kwa mwanamume. Hapo ndipo mwanamke hujipata akidhulumiwa ili apate msaada. Kijasiri baada ya kufiwa na mumewe akiwa angali kijana, alilazimika kufuatilia malipo ya mumewe katika shirika la Mamba ambalo lilimilikiwa na Kifuja pamoja na wenzake kama Angusha. Kijasiri alijaribu kufuatilia asifaulu na hapo ndipo Angusha alidai kumsaidia Kijasiri iwapo tu angekubali wawe na urafiki wa kimapenzi.

Hata hivyo Kijasiri alikuwa ni kijana mwenye maadili na ambaye alithamini heshima. Alimkabili Angusha na kumuonya asimkosee heshima zake. Alikuwa radhi kukosa malipo yale lakini atunze heshima zake na asitumiwe vibaya kama ilivyokuwa kawaida kwa wengi wa jinsia ya kike. Kupitia kwa maelezo ya Kijasiri anasema: “Hadhi yangu, utu wangu na thamani ya maisha yangu ni kuu kuliko mali.Na wakae na kesi zao na hayo malipo...” (uk 98 )

Azma kuu yake Kijasiri ilikuwa ni kuwa na jamii ambayo ingekuwa na usawa wa watu wote bila kujali jinsia umri au kabila. Alitumaini kuwa na shirika ambalo lingewahusisha wanajamii wote ambao wangejihisi kuwakilishwa.

Kijasiri baada ya kufiwa na mumewe, alijipata katika utata akiwa katika jamii ambayo ilimdhalilisha mwanamke na ilimchukulia mwanamke kama kiumbe duni. Kulingana naye hakuona tofauti ya kijinsia hasa katika utenda kazi. Aliona maonevu mengi kwa jinsia ya kike na akatamani kuwa jamii ingekuwa na wajibu wa kuwapa wanawake nafasi iliyo sawa na wanaume kwa kuwa mtazamo wa mwanamke wa jadi ulikuwa umepitwa na wakati. Tunaelezwa kuwa,

> Kijasiri alikasirika kutokana na namna baadhi ya jamii zilivyomchukulia hasa mwanamke. Kisa cha kumpiga mwenzio ati kumtia adabu! Kijasiri hakutaka kukumbuka yaliyompata Sifichi, rafiki yake. (uk 138)

Sifichi alipitia dhuluma nyingi katika ndoa yake na Mayowe. Hii ni baada ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi naye akiwa bado shuleni. Hatimaye Sifichi aliolewa na Mayowe huku akiongozwa na tamaa ya pesa alizokuwa nazo mwanamume huyu. Baada ya kuolewa Sifichi alipitia mateso mengi katika ndoa ile kiasi cha kujuta uamuzi wake wa kuchumbiwa. Ni katika hali hii yake ya kudhulumiwa ambapo Sifichi alifanya jitihada za kwenda shuleni na vibandani kuwashauri wasichana wenzake wasije wakajikuta katika hali yake. Hatimaye alijiunga na shirika la Kijasiri ambalo lilikuwa likiwatetea wanyonge na kuwalisha watoto ambao walikumbwa na changamoto mbalimbali. Sifichi alikata kauli ya kuivunja ndoa yake mradi apate uhuru na haki zake.

Katika *Zinguo la Mzuka*, mhusika wa jinsia ya kiume Zinguo anatumia nafasi yake ya uongozi wa nchi ya Kusinyika kumdhulumu kimapenzi kijakazi wake Sichana. Huyu alikuwa ni kijana ambaye alikuwa amefanya kazi kwa kiongozi huyu kwa muda wa miaka mingi. Katika harakati zake za kufanya kazi Zinguo alighadhabishwa na wimbo aliokuwa akiuimba msichana huyu. Hapo ndipo alimwamrisha achukue virago vyake na aende zake . Sichana alijaribu kueleza kuwa walikuwa wakiuimba wimbo ule katika shule ya msingi lakini Zinguo hakumpa nafasi ya kujitetea. Alipokuwa akitoka Zinguo alimshika kwa nguvu na kumwelekeza chumbani mwake. Katika chumba sauti ilisikika ya kuomba kusaidiwa kutokana na dhuluma hii. Hatimaye Sichana alitoweka baada ya kuacha kazi kwa kiongozi huyu. Katika mazungumzo kati ya Zinguo na Kaza, ni wazi kuwa kiongozi huyu alionekana akijigamba kuwa alikuwa amejifurahisha na msichana mchanga.

(...Sichana anapita karibu na Zinguo.
Zinguo anafumbua macho nakumshika mkono)
**Zinguo**: ..nilikuwa nimesahau mke wangu hayuko.
Nitakupa kazi mpya.(Wanavutana lakini
Zinguo anamshinda Sichana nguvu....kilio
Chakutakamsaada kinasikika kwa
mbali ndani) (uk 28)

Sichana ni kijana ambaye anawakilisha wasichana ambao wanapitia changamoto nyingi kutoka kwa waajiri wao hasa waajiri wa kiume manyumbani.Kupitia kwake tunaona taswira ya vijakazi ambao wanajaribu kujikomboa dhidi ya maovu wanayotendewa na wanaowaajiri. Mwandishi anadhamiria kuonyesha kwamba licha

ya umasikini alionao mtu, si lazima ajiingize katika utovu wa kimaadili. Pia anashinikiza waajiri kama Zinguo wachukuliwe hatua za kisheria ili kukomesha dhulumu kwa jinsia ya kike.

### 3.2.3Ufisadi

Katika uhalisia kuna uwiano wa kati ya yale yanayosimuliwa katika fasihi na yale na yale yanayotokea katika maisha halisi. Ufisadi si tatizo geni katika mataifa mengi. Ni tatizo ambalo huangaziwa mara kwa mara katika vyombo vya habari. Wakati mwingi ufisadi huhusishwa na viongozi walio katika mamlaka. Vijana wameonekana wakiungana na pia wakishirikiana na jamii ili kupigana na maovu haya. Mwandishi wa kazi tulizoteua vilevile ameangazia uovu huu ambao umechangia pakubwa ukosefu wa maendeleo katika katika jamii za kazi hizi. Vijana hata hivyo wamejitokeza katika kupigana na uovu huu miongoni mwa viongozi hawa.

Katika hadithi ya “Mwavyaji wa Roho” ufisadi unajitokeza kupitia kwa viongozi ambao wako katika mamlaka. Ufisadi unaoendelezwa unakuwa ni changamoto kubwa kwa wananchi ambao wanajaribu kujinasua kutoka kwa hali duni ya maisha. Ijapokuwa kila mwananchi anastahili kutafuta riziki yake halali mahali popote pale nchini, panakuwepo na kizuizi kutoka kwa viongozi wenye ubinafsi ambao nia yao ni kushibisha matumbo yao. Kitambi anapata utajiri wake kwa njia zisizo za haki. Haya tunafahamishwa na Saida kwamba baada ya magari madogo kuondolewa mjini yalikuja mabasi mengi yaliyokuwa na jina la “mzee” yaani Kitambi na ambayo yalikuwa hayafuati sheria zilizokuwa kimewekwa na utawala wa mji. Inasemekana kuwa,

> Mabasi yenyewe yalikuwa na sifa tatu tofauti na
> sheria za magariya uchukuzi nchini;hayakuwa na
> mikanda, dereva na makanga hawakuvalia sare
> na hayakusimamishwa kuangaliwa na
> maafisa wa polisi. (uk 76)

Katika hali kama hii, ni wazi kuwa baadhi ya watu kama vile Kitambi walikuwa radhi kufanya watakalo kwa kuwa walikuwa na nguvu kiuchumi. Wananchi wananyimwa nafasi ya kufanya biashara ya uchukuzi mjini ili walio na usemi wapate nafasi hizo. Pamoja na haya serikali inaonekana kushiriki ufisadi huu wanapokosa kukagua

magari haya kulingana na sheria zilizokuwa zimewekwa. Ufisadi wa aina hii unashuhudiwa katika ulimwengu halisi pale ambapo kwa kawaida huendelezwa na walio katika mamlaka. Uovu huu huendelezwa na viongozi kama hawa kwa kuwa wanatumia nafasi ambazo wamepewa serikalini wakijua kwamba si rahisi wajulikane.

Saida anadhihirisha vita vya ufisadi anapoamua kurudisha funguo za nyumba ambayo alikuwa amepewa na Kitambi ili asifichue siri kuhusu maovu aliyokuwa akiendeleza. Saida anakuwa mfano mzuri wa vijana ambao hawataki kujihusisha na viongozi fisadi ambao wananufaika kwa njia za ulaghai akilinganishwa na baadhi ya vijana katika vyuo vikuu ambao wangekumbatia uovu kama huo. Badala yake anahiari kwenda kuishi katika mabanda ilimradi asijhusishe na viongozi fisadi kama Kitambi

Jael anapata wadhifa mpya wa mkurugenzi wa maswala ya vijana kwa njia zisizo za haki kutokana na kuwa amuye Kitambi alikuwa kiongozi. Jambo hili linamsumbua Saida sana na anaonekana kupingana na hili kwa kuwa wasio na wa kuwatetea huenda basi wasinufaike na ajira kama zile. Katika uzungumzi nafsia anatueleza haya: "Nilijikuta najibizana naye. Japo yeye ndani mimi nje. Wewe nani si kijana wewe? Umefikaje huko?...." (uk 84)

Saida anapigania ukombozi wa vijana ambao umeangamizwa na viongozi ambao wamekuwa katika mamlaka kwa miaka mingi. Pia anawasuta wananchi ambao licha ya kunyanyaswa na viongozi hawa, bado wanaendelea kuwachagua na kuwaingiza katika serikali. Anaeleza kuwa vijana katika serikali ya aina hii hawana nafasi ya kuongoza ndipo anasema ",...Pesa kweli silaha...Ya kuangamiza matumaini ya watu.,hasa vijana." ( uk 84).

Katika nchi kama hii uongozi wa vijana unakuwa ni ndoto tu kwa kuwa hawawezi kupingana na wazee wenye pesa kama Kitambi katika siasa. Ingawa wananchi wana uwezo wa kuchagua vijana kupitia kwa kura, hili haliwezekani kwa kuwa wao pia wanaangalia utajiri alionao mwanasiasa yeyote yule. Ukombozi dhidi ya ufisadi utawawezesha viongozi wafaafu kupata nafasi ya kuongoza kwa njia iliyo huru. Mwandishi katika kazi hii anamulika yale yanayopatikana katika mataifa mengi barani Afrika hasa katika kipindi cha uchaguzi. Ufisadi umekuwa ukishuhudiwa

nyakati hizi wakati viongozi huwahonga wananchi ili wachaguliwe. Wananchi nao huingia katika mtego wa aina hii na kuchagua “pesa” badala ya viongozi.

Katika *Yasinya* jamii ilikumbwa na changamoto ya ufisadi kutoka kwa viongozi kama vile Kifuja. Mali aliyokuwa nayo Kifuja ilikuwa si halali. Aliunda kamati ambazo washiriki wake walikuwa ni jamaa zake huku akiwatenga wananchi ambao wangeng’amua njama zake. Kwa kuwa Kifunja alifahamu Asisi alikuwa mpiganiaji haki za jamii, aliamua kutomhusisha katika kamati na badala yake, alipendekeza Kipokeo kuchukua uenyekiti wa bodi ya usimamizi wa hazina na ustawishaji. Hii ilikuwa ni mbinu ya kumnyamazisha Asisi. Licha ya kuwa Kipokeo alikuwa ameahidiwa mshahara mnono, alitupilia mbali pendekezo hili kwa kuwa aligundua hiyo ilikuwa ni njia ya kumpumbaza ili Kifuja aweze kuendeleza ufisadi kwa manufaa yake na jamaa zake. Kwake Kipokeo alichukulia kuwa huo ungekuwa ni usaliti mkubwa kwa mwenzake Asisi. Anaeleza yafuatayo:

> ....lakini sijawahi kuwa mwenyekiti awali wala kuwa na ujuzi wa mambo ya utunzaji hazina na uratibu. Heri tumpe Asisi. Kipokeo alijibu. ...nataka uwe mwenyekiti. Mke wangu, binamu yake na yule rafiki yangu Shindo watachukua nyadhifa zilizobaki.( uk 44).

Kauli ya Kipokeo kukataa nafasi aliyopewa na Kifuja ni dhihirisho ya vita dhidi ya ufisadi ikikumbukwa kuwa Kipokeo alikuwa mwanafunzi na hakuwa na ajira kwa hivyo hii ingekuwa nafasi nzuri yake ya kupata hela za kugharamia elimu yake .

Liwazo anapinga vikali ufisadi uliokuwa ukiendelezwa na babake mzazi ambaye alikuwa na mali katika nchi za ugenini. Babake alishirikiana na mwandani wake kunyakua mali Wanamabonde. Liwazo analikataa kushirikiana na viongozi hawa na badala yake alimuasi babake na kujiunga na vijana wenzake ambao waliongozwa na Asisi kupigania haki za Wanamabonde. Kitendo hiki cha Liwazo kilikuwa ishara ya kupevuka kwa vijana ambao azma yao ni kuwaondoa uongozini viongozi wasio na maadili. “...Mwanawe, Liwazo alikuwa ameanza kumuasi na kuuungamkono upande wa kina Asisi...” (uk 60)

Asisi akishirikiana na Kijasiri waliungana kupinga maovu yaliyokuwa yanaendelezwa na Kifuja kwa kuandaa maandamano yaliyokuwa yanashinikiza kuondolewa kwa magari ya kiongozi huyu pale jijini. Kulingana na sheria za Mabonde magari ya

abiria yalikuwa hayaruhusiwi kuingia jijini kubeba abiria. Hata hivyo magari ya pekee ya kubeba abiria yaliyokubaliwa kuingia ndani yalikuwa ya Kifuja. Hali hii ilibainisha ufisadi unaoendelezwa na viongozi walio katika mamlaka.

Asisi alipokuwa kizuizini, kesi yake ilichukua muda mrefu kuamuliwa. Afisa aliyekuwa na kesi yake alidai kuwa uchunguzi ulikuwa bado unaendelea. Hatimaye ilibainika kuwa lengo la huyu Afisa lilikuwa ni kupewa hongo ili aharakishe kesi hii. Licha ya kuwa Asisi alikumbwa na matatizo mengi pale kizuizini, aliamua kuwa yeye hakuna wakati angejihusisha na ufisadi au jambo lolote ambalo halikuwa la haki. Wazazi wake Asisi walikuwa radhi kumpa Afisa yule hata sehemu ya shamba yao ili kesi hii itupiliwe mbali lakini Asisi aliyapinga haya kama tunavyoelezwa:

> Afisa huyo aghalabu alikuwa amemsihi ampe sehemu ya shamba.
> ...Lakini Asisi alizidi kukaidi na kudinda chochote ambacho
> Aliona kilikwenda kinyume na haki, maadili na sheria.... (uk 64 -65)

Ufisadi vile vile uliendelezwa katika baadhi ya mashirika ambayo yalikuwa yamepewa jukumu la kuwahudumia wananchi. Mojawapo ya mashirika haya ni Shirika la Bima la akina Kifuja wakiwa na Angusha na wengine.Ni katika shirika hili ambapo Kijasiri alikuwa akifuatilia malipo ya mumewe ambaye alikuwa ameaga dunia. Baada ya Asisi na Kijasiri kujaribu kupeleka tetesi zao katika shirika hilo, mhazili aliwaambia bila kuwaficha kuwa wangefaidika tu iwapo wangetoa kitu kidogo. Kijasiri alipinga kwa ukali sana. Hata hivyo Asisi alifanya njama ya kumrekodi mhazili huyu ambaye alikuwa anaitisha hongo. Wawili hawa walitarajia tume ingechukua hatua mwafaka kwa mhazili yule. *“....*wangu mtupu haulambwi, wewe bwana unajua ilivyo, jikune. Unapoweza, Kijasiri nusura amuume amtafune kwa meno . Kitu gani?.”....(*uk110)*

Ufisadi ulikuwa umeenea kote hadi katika asasi za kijamii kama vile shuleni. Walimu wakuu waliitisha hongo kwa wanafunzi ambao walikuwa wanajiunga na shule za msingi. Hata hivyo hili lilitendwa kwa wale ambao walionekana kuwa na uwezo kiuchumi. Kijasiri alipoenda kumtafutia mwanaye nafasi ya kujiunga na darasa la kwanza, aliambiwa ni sharti angelipa pesa za dawati na pia anunue vitabu kadhaa. Kijasiri hakusita kuuliza maswali kwa kuwa hakuelewa sababu ya haya ilhali elimu ilikuwa ni ya bure katika eneo la Mabonde. Pia mwalimu mkuu alimuuliza ampe kitu

kidogo cha kugharamia masomo ya watoto wasiojiweza. Kijasiri alipatiwa kadi ili apatiane mchango wake lakini alikataa kutoa mchango wowote. Huenda hii ilikuwa moja wapo ya mbinu alizokuwa anatumia mwalimu mkuu ili kupatiana nafasi ya kujiunga na shule ile. Kijasiri alikataa kushirikiana na mwalimu huyu na badala yake akaamua kwenda kutafuta shule kwingine.

Huku Wanamabonde wakiendelea kutaabika kwa kukosa makao, Kifuja alimiki mashamba makubwa ambayo alikuwa ameyapata kwa njia isiyo halali. Hatimaye. Kijasiri akishirikiana na wanahabari walifuatilia kwa karibu kutaka kujua njia alizotumia Kifuja kumiliki mashamba aliyokuwa ameyatwaa yauziwe maskwota.Ni kutokana na shughuli hizi za akina Kijasiri ambapo ilibainika kuwa Kifuja alikuwa anawahadaa wananchi kwa kuuza mashamba yale kwa bei ya juu sana. Alipokabiliwa na Kijasiri na wanahabari kuhusu ununuzi alikuwa na haya ya kusema: “ Kulikuwa na makubaliano baina ya muuzaji na mnunuzi.........." (uk 63)

Baadaye Kijasiri pamoja na wenzake walishirikiana wakanunua shamba ili kuwapa wananchi waliokuwa hawana makao. Walinunua kwa bei ya chini badala ya bei ya juu kutoka kwa Kifuja ikikumbukwa kuwa mashamba ya Kifuja yalikuwa yamenyakuliwa kutoka kwa umma. Kijasiri aliwaepushia Wanamabonde hadaa ya Kifuja ambaye kusudi lake lilikuwa ni kujinufaisha pamoja na aila yake.

Kifuja ni kieleezo cha viongozi katika mataifa baadhi ya mataifa ambao wamejinufaisha kwa njia zisizo za haki. Uovu huu umelemaza maendeleo ya nchi nyingi huku watawaliwa wakiendelea kutatizika na kutozwa kodi za juu ambazo haziwanufaishi. Ni kweli kuwa kesi nyingi za ufisadi huwahusu viongozi katika jamii ni nadra kuona mwananchi wa kawaida akihusishwa na ufisadi wa mali ya umma kwa kuwa hana nafasi.

### 3.2.4 Ukombozi wa kimawazo

Hii ni hali ambapo mtu anakuwa na mawazo yaliyo huru hivi kwamba hawezi kuathiriwa na mawazo potovu kama vile tamaa ya kupata mali kwa njia zisizo za haki au hata kushiriki katika anasa ambazo ni zao la maovu yanayopatikana katika jamii.Mtu anapokombolewa kimawazo anaweza kuyatathmini mambo kwa njia isiyo

ya kawaida au iliyozoeleka hali inayomwezesha kuwa na mtazamo tofauti na baadhi ya mambo yanayochukuliwa kama kaida.

Kupitia kwa Saida, mwandishi anayaangazia maovu ya viongozi katika bara la Afrika. Saida ni kijana ambaye amejikomboa kimawazo na ambaye ana mtazamo tofauti kabisa na vijana wenzake ambao wamejiingiza katika maovu wakiwa na mtazamo wa kupata hela. Kutokana na haya vijana kama hawa wanashirikiana na viongozi waovu bila ya kuwazia kuhusu mienendo yao .Kupitia kwa mawazo ya Saida, anakereka na ukosefu wa maadili miongoni mwa viongozi katika Afrika. Licha ya maovu waliyonayo viongozi hawa, hakuna hatua ya kisheria inayochukuliwa dhidi yao tofauti na ilivyo katika mataifa ya Ulaya.

Saida anasononekea hali ya vijana ambao wanashiriki madawa ya kulevya na kuwafanya wakose matumaini ya maisha. Ni katika hali hii ambapo Saida anaamua kukatiza urafiki wake na Jael licha ya ahadi alizokuwa ameahidiwa. Anawalaumu wananchi ambao wanawachagua viongozi kama Kitambi kwa sababu ya pesa wanazowapa wakati wa uchaguzi.

Mhusika Saida ni kiwakilishi cha vijana waadilifu katika ulimwengu halisi. Licha ya kuwa idadi kubwa ya vijana katika vyuo vikuu hujihusisha na maovu ya kila aina, bado kunapatikana vijana ambao ni waadilifu na wenye mawazo huru hivi kwamba wao ndio wanaibuka kufichua maovu yanayoendelea na kujaribu kutafuta suluhisho.

### 3.2.5 Ukombozi wa kisiasa

Nadharia ya uhalisia inasisitiza kuwa fasihi ni kioo cha jamii kwa hivyo sharti kazi yoyote ile ya fasihi iiangazie jamii kama ilivyo. Vijana katika miaka ya hivi karibuni wameonekana wakishiriki pakubwa katika siasa za nchi. Serikali pia imewatengea vijana nafasi yao ili wawe na wawakilishi wanaowasilisha masuala yao. Ni kutokana na haya ambapo mwandishi wa kazi tulizoteuwa amewamulika vijana katika uwanja huu wa siasa.

Ukombozi wa kisiasa katika kazi hizi ni hali ambapo taifa au hata jamii hujaribu kujinasua kutokana na minyororo ya utawala wa waafrika ambao walirithi utawala kandamizi wa kikoloni. Katika eneo hili la Kitambi wananchi wanaonekana

wakihadaiwa kuendelea kuwachagua viongozi kama Kitambi licha ya kuwa walielewa fika viongozi hawa hawakustahili kuwaongoza. Ilipotokea yeyote aliyekuwa anampinga kiongozi huyu “suluhisho” la haraka lilipatikana la kumwangamiza ili kulemaza upinzani wowote. Hili lilimtendekea mpinzani mmoja ambaye alikuwa amependekezwa na baadhi ya vijana kama vile Saida. Ilipobainika kwamba mpinzani huyu alikuwa na nafasi bora zaidi kuliko Kitambi, njama ilipangwa na mpinzani huyu akatoweka kwa muda hadi pale siku zilipita za kuwasilisha karatasi za uteuzi. Hii ilikuwa ni njama ya kuhakikisha Kitambi angechaguliwa wananchi wapende wasipende kwa kuwa hakuwa na upinzani wowote.

Saida pia anadhihirisha kuwa watu katika jamii hii hawakuwa na haki ya kuchagua viongozi wa kisiasa waliowapenda. Hii inajitokeza wakati mama mjamzito alipigwa hadi kuavya kwa kuwa alikuwa anapinga kuchaguliwa tena kwa mzee Kitambi. Saida anapinga kitendo hiki cha unyama alichofanyiwa mama huyu hadi anarejesha vitu alivyokuwa amepatiwa na Kitambi. Anatueleza yafuatayo: “Nilichokiona dhidi ya mama mjamzito ndicho kilichobadlili mawazo yangu na hata nikazirudisha funguo za nyumba niliyopewa kule ukwasini”(uk 81)

Nchi zinazodhamini haki huwapa wananchi wao nafasi ya kuchagua viongozi wanaowapendelea bilakuwashinikiza.Kitendo cha unyama cha kumvamia mama mjamzito kwa sababu ya kutetea haki ya kidemokrasia kilighadhabisha watu wengi. Saida anatambua haja ya dharura ya kuwaondoa mamlakani viongozi wa aina hii.

Jamii ya Kusinyika ilikumbwa na changamoto za uongozi mbaya kutoka kwa waafrika walioshika hatamu ya uongozi baada ya kupata uhuru. Wakiongozwa na Zinguo pamoja na Kaza, viongozi hawa waliendelea kushirikiana na wakoloni kuendelea kuifilisi Kusinyika ili wao wenyewe waendelee kufaidika. Zinguo kama kiongozi ambaye alikuwa ameaminiwa kuilinda katiba ya Kusinyika, alikuwa anawalaghai wananchi walete mazao na hata mifugo akidai kuwa alikuwa anatoa kafara kwa Mizuka. Hili linajitokeza katika usemi wake Zinguo. Anawaambia watu:

Mizuka hawabanduki bila kafara; haya!
Leteni kafara. Nataka magunia ya nafaka, mchele,
ngano na mahindi. Magunia mengi! Nataka mbuzi
kondoo na ng'ombe. Leteni hata ngamia na punda
kama wapo.Leteni! (uk 49)

Hata baada ya watu kuleta walivyoitishwa, hali yao ya kimaisha iliendelea kuwa mbaya. Watu waliendelea kulalamika na kunung'unika kwa kuwa hawakupata huduma bora au hata kupata waliyokuwa wameahidiwa na Zinguo. Badala yake Zinguo aliendelea kujinufaisha pamoja na kiongozi mwenzake Kaza kama inavyojitokeza katika mazungumzo yafuatayo:

**Zinguo** : Mimi!
Nitayatwaa mashamba na kuwapa watu wetu!
Kabila langu na lako pia; magari biashara na....
Tumetajirika Kaza!....
**Kaza** : Utamu wa kuongoza!
Ni sisi tunawika, wao juu yao kutenda.
Hiyo ndiyo kazi ya watwana na mayaya.. (uk 30)

Vijana waliungana na wanakusinyika kupigania ukombozi wa nchi yao. Hii ni baada ya kuona jinsi hali ilivyokuwa katika uongozi wa Zinguo.Wakiongozwa na Mtu 1 na Mtu 2 Wanakusinyika walianza kubainikiwa na hali kama ilivyokuwa.

**Mtu 1** : Mnanyolewa jamani!
Msikubali kuhadaiwa tena1
**Mtu 2** : (Anasisitiza ya mwenzake) ......Torokeni
Jamani ! Zinguo anatutumia kuvuruga vitu nchini.
Anatuzika tungali hai ! (uk 32)

Hatimaye Mtu 1 na Mtu 2 waliwaunganisha Wanakusinyika pamoja bila ya kujali tofauti za kikabila wala kijinsia ili kuung'oa uongozi wa Zinguo. Haya yanajitokeza kutoka kwa Mtu 1 anaposema:

**Mtu 1** : (Taratibu) Kipindi kimepita kirefu
Hata hivyo tunaweza kujenga nchi yetu upya
Bora ari. Bora umoja. Umoja ni nguvu.
Bora tukatae kutenganishwa!
Tusiwabague wenzetu kwote katika
Kusinyika. (uk 76)

Vijana wa Kusinyika walisaidiana na Askari kushika doria baada ya Zinguo na Kaza kushikwa na kutiwa gerezani. Vijana pamoja na Askari waliwalinda Zinguo wasije wakaokolewa na wafuasi wao ambao sasa walikuwa matatani. Mwandishi amewapa vijana nafasi hii kuonyesha kuwa vijana wanapaswa kuhusika katika kutatua matatizo yanayoikumba jamii. Mchango wa vijana unabainika katika nukuu ifuatayo.

> ...Ndani walimofungwa Zinguo na Kaza....
> ....Askari, vijana wa kike na wa kiume wamekaa
> na kushika doria.Mmoja ametazama kushoto na
> mwingine kulia....(uk 87)

Baada ya kuwashinda Zinguo na wafuasi wake, Wanakusinyika walikusanyika pamoja na kufurahia ushindi na juhudi zao. Mtu 1 alipendekeza wakutane baadaye na kuchagua viongozi ambao wangeongoza kwa uadilifu. Ilibainika kuwa hata vijana wangeweza kuongoza iwapo wangepatiwa nafasi kama anavyoeleza Mtu 1:

> **Mtu 1 :**.... Mimi nashikilia tu, juu yenu sasa kumtafuta
> Mtu mwenye uwezo.Na mzalendo kuchukua usukani!
> Tuna vijana na wazee wenye hekima ya
> kushauri vijana wetu...... (uk. 96)

Haya yanadhihirisha kwamba kuna haja ya kuwa na watu watakaowajibikia kuwashauri vijana ambao hawana mwelekeo katika jamii. Miongoni mwa washauri ni vijana wenzao lakini walio na maadili. Kwa mujibu wa haya ni dhahiri kuwa ili kuwa na jamii imara ni sharti vijana wawe waadilifu na pia wawe katika mstari wa mbele kupigania jamii zao.

Mwandishi wa kazi hizi amewatumia wahusika vijana kuwakilisha uhalisia katika jamii ambapo wakati huu vijana wengi wameonekana wakiitosa katika siasa na kuwapinga viongozi wakongwe. Baadhi yao wamefanikiwa na hata wamepata nafasi kama wawakilishi wa wananchi. Tofauti na siasa za nchi vijana vilevile hushiriki siasa katika maeneo mengine kama vyuo vikuu na kwa hivyo hali hii ya siasa ni ya kiuhalisia miongoni mwa vijana.

### 3.2.6 Ukoloni mamboleo

Licha ya mataifa ya Afrika kupata uhuru baada ya utawala wa mkoloni, mataifa ya ughaibuni yangali yanadhihirisha ushawishi mkubwa katika bara ya Afrika.

Mwandishi ameyaangazia haya katika *Zinguo la Mzuka* kupitia kwa mhusika Sichana kijana wa kike aliyekuwa akifanya kazi ya ujakazi kwa kiongozi wa kiafrika aliyejulikana kama Zinguo. Katika wimbo wake Sichana, sauti ya kulilia ukombozi wa bara la Afrika inasikika. Ni sauti ambayo inahuzunisha na ambayo inasikika kutoka kwa mtu ambaye anaomboleza**.** Sichana katika sauti yake anaomboleza hali ya Afrika kuendelea kunyonywa na mataifa ya ughaibuni na kwa hivyo kuwafaidi wageni huku wenyeji wakiendelea kutaabika.

Unalisha wa mbali na wakaribu
Madini yako
Wanyama wako fahari yako
Mito yako.....
Lakini ?
Umevuliwa nguo
Umeachwa uchi
Unalisha wa ughaibuni ......
Mimi mnyonge nanyongeka uchao. (uk 25)

Kilio hiki ni ishara kuwa mataifa ya ughaibuni yananufaika na rasilimali za Afrika kama vile madini pamoja na uwindaji haramu ambao umesababisha kuangamia kwa wanyama wa pori , huku Waafrika wakiendelea kuumia na kung’ang’ania rasilimali chache ambazo zimebaki. Sichana katika kilio chake anawazindua waafrika kwa kuwatahadharisha kwamba ukoloni mamboleo ni mojawapo wa changamoto kubwa ambalo linastahili kutafutiwa suluhisho la haraka lau sivyo waafrika wataendelea kuwa masikini na kuyategemea mataifa haya ambayo yanachukua utajiri wao na kujinufaisha nayo. Ukoloni-mamboleo ni hali ambayo inaweza kudhihirika katika mataifa mengi yanayoendelea. Hali hii hutokana na kuwa mataifa haya hayawezi kuyakithi mahitaji ya wananchi wao kwa hivyo yanajipata yakiendelea kuyategemea mataifa ya ughaibuni.

### 3.2.7 Unyanyasaji wa wafanya kazi

Japo Sichana ni kijana wa umri mdogo, analilia ukombozi wa wafanyakazi au wahudumu katika nyanja mbalimbali. Yeye kama mfanyakazi wa nyumbani, anawakilisha wafanyakazi ambao wanapitia dhuluma nyingi kutoka kwa waajiri wao na kwa hivyo wimbo anaoimba Sichana ni dhibitisho la mtu ambaye analilia ukombozi wa wanaonyanyaswa ili waweze kutendewa haki kama binadamu wengine.

Ingawa wafanyakazi wanafanya kazi ya kuchosha, wao wanalipwa mishahara duni kama inavyojitokeza katika wimbo huu.

Mimi ndiye hayawani wa huduma
Naandaa meza nisiyoila.Lakini ?
Mzigo nabeba mimi
Utwana ni wangu
Ujakazi ni wangu
Ujira wangu japo mkonde
Natoa za utendaji. (uk 26)

Wimbo huu unawarejelea wafanyakazi ambao kila uchao wanalalamikia mishahara wanayolipwa baada ya kufanyishwa kazi ya sulubu. Licha ya hayo wafanyakazi hawa wanatozwa kodi ambayo inaishia katika mifuko ya viongozi katika utawala. Huu ni wito kwa wafanyakazi waungane ili waweze kujikomboa kutokana na dhuluma hizi. Kulingana na mtazamo wake Sichana, kuna haja ya wafanyakazi hasa wa nyumbani kupewa heshima zao na kuwachukulia kama binadamu wengine.

### 3.2.8 Ukombozi wa Kimaadili

Maadili ni hulka njema pia ni mienendo inayokubalika katika jamii fulani kulingana na utamaduni wake. Asisi kijana aliyekuwa ametoka chuo kikuu alikuwa kielelezo kizuri cha vijana wenye maadili katika jamii. Alikuwa hajihusishi na maovu yatendwayo na vijana wa umri wake. Ijapokuwa Asisi alifanya kazi katika viwanda, yeye hakushiriki maovu. Aliweza kujikomboa kutokana na waliyoyatenda wafanyakazi wenzake.

Tangu aajiriwe viwandani E.P.Z na tangu
apande daraja na kufikia
kiwango cha msimamizi, hakula hongo
wala kufuatana na msichana
pale viwandani.....Hakujaribu.
Alijiheshimu wakamheshimu......(uk18)

Alipomtembelea Kipokeo Athi River karibu na mtaa wa Changu Kidogo, Asisi alitoa noti na kumpa Kipokeo na baadaye wakaanza kula mayai. Kitendo hiki kiliashiria tayari Asisi alikuwa ameanguka mtego wa kushiriki ukahaba na Kipokeo kwa kuwa hii ndiyo sifa ya sehemu hii. Hatimaye wawili hawa walianza mazungumzo kuhusu maisha yao ya hapo awali, kila mmoja akisimulia mwenzake changamoto alizokuwa amekumbana nazo katika maisha. Jambo hili halikuwa la kawaida kwa wateja wa

Kipokeo ambao waliwahi kuingia chumbani mwake. Asisi basi alikuwa wa kipekee. Mwandishi anatueleza kwamba:“Kipokeo alishangaa sana. Alikuwa hajawahi kupata mteja wa namna ile. Hana pupa, hana njaa ya raha wala kiu ya ufuska....”(uk24)
Baada ya mazungumzo baina ya Kipokeo na mteja wake jambo lililotarajiwa kufuata kwa kawaida lilikuwa ni wawili hawa kuzini kama alivyokuwa amezoea Kipokeo mara tu alipomwona mwanamume katika chumba chake. Hata hivyo hili halikuwa kwa kuwa Asisi aliomba kuondoka ili arudi makaazi yake. Tofauti na vijana wenzake Asisi alikuwa ni mwenye maadili jambo ambalo Kipokeo hakulitarajia. Alibakia kama ameduwaa kutokana na mazungumzo waliyokuwa nayo na kijana huyu.

Mazungumzo waliyokuwa nayo, yalileta mabadiliko makubwa katika maisha ya Kipokeo kwa kuwa baada ya muda mfupi Kipokeo naye pia alijikomboa na kuwa mwadilifu hadi akarudi kuendelea na masomo yake.

### 3.2.9 Uharibifu wa mazingira

Mazingira ni muhimu katika maisha ya kila siku na kwa hivyo kuna haja ya kuyatunza mazingira. Utunzi wa mazigira ni hali ya kuhifadhi mazingira asilia kupitia kwa mashirika, serikali au kwa misingi ya mtu binafsi. Haya yote ni kwa manufaa ya jamii. Kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira umeongezeka kutokana na wingi wa watu na hata teknolojia kwa mfano ujenzi wa barabara na hata reli. Ni kwa sababu hii ambapo kuna haja ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

Katika *Yasinya*mwandishi ametuonyesha jinsi mazingira yameharibiwa kwa manufaa ya watu binafsi huku matokeo yakiwa ni athari mbaya kwa jamii kama vile kukauka kwa mito na hatimaye ukosefu wa mvua ambayo imesababisha kuwepo kwa ukame. Kijasiri katika mawazo yake anakereka kuona mazingira yameharibika na hakuna yeyote anayeshughulika kuyahifadhi. Kulingana naye, uharibifu wa mazingira ni sawa na kuibaka au kuinyanyasa Afrika. Kupitia kwa mawazo yake tunaelezwa:

> Hawa ndio wanaoitwa wabakaji na
> wanyanyasaji wa mama
> Hivi haya magogo, hawaoni
> ukali wa jua hili? Nusura
> tutaanza kuishi jangwani,
> aliwaza..... ( uk40)

Kijasiri aliwaza zama ambazo mazingira yalikuwa hayajaharibiwa na hili lilimfanya kusononeka. Msitu wa Namunyiri ulikuwa mkubwa na wanyama anuwai walipatikana mle. Mto Nzoia nao ulikuwa na samaki ambao waliwashibisha wakaazi. Leo hii Kijasiri alifadhaika kwa kuwa Mabonde ilikuwa inabadilika kuwa jangwa. Katika juhudi za kupigania ukombozi wa mazingira Kijasiri alishirikiana na watu kama Profesa Amazulu aliyekuwa mwanamazingira mashuhuri katika kuwashauri Wanamabonde kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

### 3.2.10 Dhuluma kwa wafungwa

Mwandishi ameangazia dhuluma wanazopitia wafungwa katika *Yasinya.* Wafungwa katika eneo la Mabonde walikumbwa na maonevu na ukosefu wa haki zao walipokuwa wamewekwa vizuizini. Mhusika Asisi ni mmoja wa wale walikuwa wamewekwa kizuizini na baadaye kufungwa jela kwa kosa lisilojulikana au kuwa na ushahidi wowote. Alikuwa amesingiziwa kuwa alihusika katika mauaji ya mhadhiri mmoja wa chuo chao.  Hata baada ya wahadhiri na marafiki kujaribu kufuatilia kosa alilolitenda, bado Asisi alisingiziwa makosa bila ya uchunguzi wowote kufanywa.

Baada ya Asisi kutumikia kifungo chake, mwenzake Anao naye alitiwa mbaroni kwa kuwa alipinga uongozi dhalimu wa babake mzazi pamoja na Kifuja.  Alipinga njama ya babake na Kifuja kuendeleza biashara ya kuuza mbao. Anao alikuwa akipigania haki za wanyonge waliokuwa wananyanyaswa na hapo ndipo alipowekwa ndani. Hatimaye Asisi waliandamana na Kipokeo hadi kituo cha polisi ili kujua yale Anao alikuwa ametenda. Wawili hawa walishinikiza Anao aachiliwe au ahukumiwe..Mwandishi anatueleza yafuatayo: "...Alipomwona Asisi na wenzake, aliduwaa. Hata Anao-hakuamini kama Asisi angekuwa na hamu ya kufuatilia kesi yake" (uk 81)

Haya yalisababisha wao kuwekwa kizuizini. Kwake Asisi alitaka haki itendeke kwa kila mtu kulingana na sheria za mabonde. Asisi alipowekwa ndani na wenzake, jaji Kata alikataa kuwapa bodi kwa tuhuma eti wangevuruga uchunguzi na  mashahidi.

Kijasiri alipokuwa kizuizini vijana wenzake walifanya kila wawezalo ili kuhakikisha kuwa haki ilitendeka.Walimtafuta wakili ambaye alikuwa akimtetea Kijasiri. Kipokeo, Asisi na vijana wengine waliungana ili kuhakisha ukweli umejidhihirisha kutokana na tuhuma alizokuwa amewekewa Kijasiri. Pia walienda kumzuru Kijasiri kila wakati katika kizuizini alimokuwa amefungiwa.Walimpa moyo na pia wakamfahamisha kuwa bado walikuwa wanaendeleza shirika lao la kupigania haki za watoto licha ya kutokuwepo kwake.

Ni wazi kuwa Wanamabonde walikuwa wamenyimwa haki zao na sheria haikutekelezwa kama ilivyofaa. Wengi wa vijana ambao walijaribu kutafuta ukweli fulani walijipata vizuizini. Pengine mahakama ingekuwa kitulizo kwao lakini hili halikuwa hivyo. Majaji pia walishirikiana na viongozi dhalimu kuwanyima haki wananchi. Kusudi la Asisi na wenzake lilikuwa kuendeleza juhudi la kuwang’oa mamlakani waliokuwa wanawanyanyasa Wanamabonde.

Hali ya wafungwa korokoni na hata vizuizini inawakilisha uhalisia katika hali ya kawaida. Baadhi ya wafungwa katika magereza hawatendewi haki na wanaowalinda. Wengine huonekana wakilalamikia mazingira wanamoishi na hata kudhulumiwa wakiwa mle ndani. Wananchi wengine hujipata wakihukumiwa kwa makosa ambayo hawakutenda huku wengine wakiwa ni washukiwa tu.

### 3.2.11 HITIMISHO

Katika sura hii ya tatu, tulichanganua aina mbali mbali za ukombozi ambazo zimefanikishwa na vijana katika kazi tulizoteua. Aina hizi za ukombozi ni pamoja na: ukombozi dhidi ya umasikini, ufisadi, dhuluma kwa wanawake, dhuluma kwa wafanyakazi, madawa ya kulevya, uasherati, ukoloni mamboleo na hata dhuluma kwa wafungwa.

Uchanganuzi wetu ulibainisha kuwa mengi ya maudhui katika kazi hizi tatu yanaingilia kwa karibu sana. Vijana wamechangia pakubwa katika jitihada za kuzikomboa jamii zao kutokana na changamoto zinazopitia. Hata hivyo kuna baadhi ya aina zingine za ukombozi ambazo ni za kipekee katika kazi hizi tatu. Aina hizi tulizichanganua zikiwa kivyake.

Wahusika vijana wamelidhihirisha uwezo wao mkubwa walipoungana na kushirikiana kuwapinga viongozi dhalimu katika harakati zao za kupigania ukombozi

# SURA YA NNE

# CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA VIJANA KATIKA HARAKATI ZA KULETA UKOMBOZI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, tuliangazia jinsi vijana walihusika katika juhudi za kuleta ukombozi katika kazi tulizoteua. Pamoja na kuwa vijana walijitahidi kutimiza azma yao, walikumbwa na changamoto mbalimbali ambazo tutazichanganua katika sura hii ya nne.

## 4.2 Changamoto katika kazi Husika

Katika kazi tulizoteua vijana wanakumbwa na vizingiti mbalimbali wakiwa katika harakati za kupigania ukombozi katika jamii zao, mwandishi anaangazia changamoto kadha wa kadha ambazo zinamkumba vijana hawa. Changamoto zenyewe ni kama vile : usaliti,  umasikini, vitisho, sheria dhaifu , kutiwa korokoni, matumizi mabaya ya mamlaka na  kutowajibika kwa maafisa wa polisi. Mbatia (2001) anasema wasanii walioshughulikia nadharia ya uhalisia waliamini kwamba ukweli uliweza kupatikana katika maisha pamoja na shughuli za kawaida za kila siku za mwanadamu katika mandhari yake ya uhalisia. Kulingana na haya ni wazi kuwa changamoto tulizozishulikia katika sehemu hii zinaweza kuhusishwa na ukweli ulioko katika maisha ya halisi. Ni masuala ambayo yanaweza kubainika katika jamii ya kawaida kwa hivyo yanachangia katika kulemaza juhudi za vijana za kuleta ukombozi.

### 4.2.1 Usaliti

Mohammed (1995) anaeleza kwamba katika uhalisia kuna uwiano kati ya yale yanayosimuliwa katika fasihi na yale yanayotokea katika maisha halisi. Mhimili huu unatumiwa kuonyesha kuwa usaliti si jambo geni katika jamii halisi na kwamba wanaowasaliti vijana katika kazi tulizoteuwa wanawakilisha binadamu wasaliti katika hali halisi ulimwenguni. Vijana katika kazi hizi wanasalitiwa na vijana wenzao pamoja na wananchi wengine. Katika maisha halisi marafiki na hata jamaa ya mtu wanaweza kuwa wasaliti katika jitihada za kusuluhisha tatizo fulani.

Ili ukombozi ufaulu kuna haja ya kuwepo kwa ushirikiano miongoni mwa wanajamii au watu ambao wanakumbwa na hali isiyoridhisha. Hata hivyo Saida alipata changamoto kubwa kutoka kwa vijana wenzake.Baadhi ya vijana kama vile Jael walilemaza juhudi za ukombozi kwa kuwa wao ndio walishirikiana na akina Kitambi kuendeleza biashara haramu ya ulanguzi wa madawa ya kulevya. Jael akiwa katika chuo kikuu alikuwa akibeba madawa haya na kuwapelekea vijana wengine na kuwauzia.Vijana hawa walikusanyika kwake wakiwemo hata wa shule za upili na wengine wa shule za msingi.Licha ya kuwa Saida alikuwa haridhishwi na mienendo ya Jael, juhudi zake zilikuwa zinalemazwa na Jael ambaye alienda kinyume na maazimio yake ikikumbukukwa kuwa yeye Jael alikuwa na ushawishi mkubwa kwa vijana wenzake.

Usaliti pia ulikuwa changamoto kubwa katika juhudi za kuikomboa jamii ya wanakusinyika. Vijana wanaungana na wananchi wengine ili kuikomboa nchi yao mikononi mwa viongozi dhalimu kama vile Zinguo. Wanapanga mikakati ya kumtimua Zinguo pamoja na wafuasi wake katika mamlaka. Hata hivyo baadhi ya vijana wanajitenga na kuamua kuunga mkono uongozi mbaya wa Zinguo. Hawa waliusifu uongozi wa Zinguo na walikuwa tayari kufanya lolote ili wahakikishe hakuna aliyempinga kiongozi wao. Usaliti unakuwa changamoto kubwa kwa kuwa vijana hawa wasaliti wanaungana na Zinguo kuendeleza unyanyasaji badala ya kuungana na wenzao kupigania ukombozi. Hali hii hujitokeza katika jamii halisi ambapo baadhi ya vijana ndio wanakuwa vibaraka wa viongozi dhalimu. Badala ya kuunga wenzao mikono wanahadaiwa kwa pesa na ahadi za uongo ili wawasaliti wenzao ambao wako katika hali ya kujinasua.

Kaza kama kiongozi aliyechaguliwa na wananchi ili awawakilishe pia anawasaliti Wanakusinyika kwa kushirikiana na Zinguo kuendeleza uongozi dhalimu. Badala ya kuwajali waliomchagua Kaza anajilimbikizia mali pamoja na jamii yake na kudai kuwa huo ulikuwa ni wakati wao walokuwa katika mamlaka. Anazificha siri za Zinguo pamoja na uhusiano wake na Mzuka. Katika mataifa mengi ambayo hayasisitizi uwajibikaji, mhusika huyu anawakilisha wananchi ambao huwa karibu sana na viongozi kama vile wafanyakazi katika afisi za umma. Watu hawa mara nyingi huelewa maovu ambayo yanatendwa na viongozi waliochaguliwa lakini badala

ya kuchukua hatua ya kuwashtaki, wao pia huwasaliti wananchi kwa kupata kilichochao mradi tu wataficha maovu haya. Hali hii hushuhudiwa sana miongoni mwa watu ambao wanasimamia miradi mbali mbali ya serikali.

### 4.2.2 Kutowajibika kwa maafisa wa polisi

Katika nchi ambayo ina sheria, maafisa wa polisi mara nyingi hutegemewa kuhakikisha wananchi wanafuata sheria kama inavyofaa. Ni jukumu la afisa wa polisi vilevile kuhakikisha kwamba wanaovunja sheria wanachukuliwa hatua ili kuhakikisha usawa katika jamii. Hali ni tofauti katika uongozi wa Bwana Kitambi ambaye alishirikiana na maafisa wa polisi kuendeleza uongozi mbaya kwa wananchi. Kwa mfano baada ya Jael kupatikana na madawa ya kulevya na kutiwa kizuizini, Bwana Kitambi alihitaji tu kuzungumza na mkuu wa polisi kupitia kwa simu na hatimaye Jael akawachiliwa huru na kurudishiwa kifurushi alichokuwa amekamatwa nacho. Afisa huyu anaahidi kuwa hili lilikuwa si kosa lake na kwamba halingerudiwa tena. Kama anavyosema "Mbona hukuniambia wewe ni mpwa wa Mzee? Wajua hawa vijana wangu wametoka mafunzoni tu juzi na hawajui kazi yao..."( uk 76)

Maneno haya ya afisa yanaonyesha wazi kuwa maafisa wa polisi wanaungana na watu kama Kitambi kuendeleza maovu badala ya kuwachukulia hatua kisheria. Ni mazungumzo ambayo yanaashiria watu wanaojuana na ambao wanafahamiana vyema. Vilevile ni wazi kuwa kuna wale ambao wanafuata sheria ilihali wengine hawafuati.

Katika ulimwengu halisi tunawaona viongozi kama hawa ambao wanahusika na maovu ya aina ila uchao wakishirikiana na askari ambao hawajawajibika katika kazi zao. Hatimaye askari hawa hudai "kitu kidogo" ili kazi iendelee. Hali kama hii inakuwa ndicho kiini cha ongezeko la uhalifu miongoni mwa jamii.

### 4.2.3 Umasikini

Donna (2007) anasema kazi za kifasihi zinapaswa kuangazia masuala ya jamii kama yalivyo katika hali halisi. Mwandishi wa kazi tulizoteua ameangazia masuala ambayo yanaikumba jamii katika ulimwengu halisi. Kati ya masuala haya ni umasikini ambao kwa uhakika umechangia pakubwa katika kulemaza juhudi za vijana za kuleta ukombozi.

Umaskini miongoni mwa Wanakusinyika ni changamoto kubwa kwa juhudi za kuleta ukombozi dhidi ya unyanyasaji hasa wa wafanyakazi. Sichana ambaye anasemekana amefanya kazi kwa Zinguo yapata miaka kumi na mitatu hivi, anaonekana akielewa hali yake ya kunyanyaswa. Hata hivyo ufukara ulioko nyumbani kwao unamlazimu aendelee kujikaza angalau wadogo wake wapate chakula na mavazi. Ni umaskini huu unamlazimu aendelee kufanya kazi licha ya malipo duni na vile vile mwajiri wake kumbaka akiwa na uhakika kwamba wazazi wa Sichana hawakuwa na uwezo wa kumchukulia hatua yoyote kisheria.

Kaza mfuasi wa Zinguo anaahidiwa uenyekiti katika tume ya kupigana na ufisadi. Hili linamfurahisha Kaza kwa kuwa anaelewa fika kwamba umaskini ungemwondokea iwapo angeshirikiana na Zinguo. Kiongozi huyu alikuwa anafahamu hali ya Kaza na kwa hivyo nafasi aliyokuwa anampa ilikusudia kumnyamazisha ili Kaza asitoboe siri zake Zinguo.Hili lilimwezesha Zinguo kuendeleza uongozi wake dhalimu kwa Wanakusinyika.

Umasikini miongoni mwa vijana na hata wananchi kwa jumla umedhihirika katika kazi hii. Hali hii ya wananchi inakuwa kikwazo kwa Saida katika kuleta ukombozi dhidi ya viongozi dhalimu na waovu. Saida anawaza ni vipi wananchi wanaendelea kuwachagua viongozi wasio waadilifu mwaka baada ya mwaka. Mmoja wa wazungumzaji anadai kuwa watu huchagua pesa wala si maadili.

Katika mkutano wa kisiasa aliohudhuria Kitambi, vijana wanaonekana waking'ang'ania fulana na hata mabunda ya noti yaliyokuwa yamebebwa na wafuasi wa Kitambi.Wamama wanaonekana wakikimbia huku wamejifunga maleso yaliyokuwa yameandikwa jina la Kitambi. Wananchi katika hali hii ya uchochole wanalazima kumchagua Kitambi ambaye anawapa pesa wakati ule kuliko mpinzani wake aliyekuwa mwadilifu. Hii inakuwa ni changamoto kubwa kwa Saida ambaye kulingana naye angemchagua mpinzani wa Kitambi. Maoni haya yake hayaungwi mkono na vijana wenzake wala majirani wake na kwa hivyo inakuwa vigumu kuwashawishi watu kama huyu kwamba bora kumchagua mwenye maadili kuliko mwenye pesa. Hali yao inawazuia kuona maisha ya baadaye.

Matukio kama haya yanadhihirika katika jamii zetu hasa katika vipindi vya uchaguzi. Viongozi hutumia pesa zao wakijua wanacholenga. Vitendo vya viongozi "kuwazawadi" wapigakura kwa maleso, pesa na hata mavazi mengine si jambo geni katika jamii yetu. Wananchi wanaohadaiwa mara nyingi huwa ni wale wa mapato ya chini au vijana ambao hawana ajira.

**4.2.4. Vitisho**

Juhudi za kukabiliana na viongozi dhalimu zinalemazwa vilevile na vitisho kutoka kwa viongozi kama vile Kitambi ambao wanaendeleza biashara haramu ya madawa ya kulevya yanayowaathiri vijana. Hata baada ya wazazi kulalamika suluhisho halipatikani la kuwaokoa wanao. Ni katika vituo vya polisi ambapo wanyonge wanatarajia kupata haki zao wanapokandamizwa. Hata hivyo hii ni kinyume na hali ilivyo katika uongozi wa bwana Kitambi. Baada ya mpwa wake Jael kutiwa kizuizini kwa kupatikana na madawa ya kulevya, afisa mkuu wa polisi alipewa onyo na kuambiwa akimye iwapo alitaka kuhifadhi kazi yake. Jael vilevile hakusahau kumwonya Saida kwamba asimwambie yeyote kuhusu yaliyokuwa yametokea.

Vitisho hivi vilikuwa ni vya kuwatia hofu maafisa wa polisi ambao walikuwa na jukumu la kuzuia matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa wananchi. Kando na vitisho Jael alikuwa amempa Saida nyumba ya kifahari katika mtaa wa mabwenyenye. Hatimaye Saida alihatarisha maisha yake kwa kurejesha funguo za nyumba ile kisha akaenda kukaa katika vibanda. Vitisho kutoka kwa Kitambi na mpwa wake viliwawezesha kuendeleza biashara yao haramu huku maafisa wa polisi wakinyamaza kwa kuhofia kupoteza kazi zao.

Askari ambao walihitajika kulinda usalama wa wananchi ndio waliotumiwa kuwahangaisha wananchi. Baada ya Asisi kutiwa mbaroni na kukaa kwa muda mrefu askari walimtisha kwa kumwambia angeozea gerezani iwapo hakuwapa hongo ili kesi yake iharakishwe. Askari hawa pia waliwatisha marafiki na hata wahadhiri waliomtembelea Asisi pale kizuizini ili wasipate nafasi ya kufuatilia kesi ya Asisi. Walipojaribu kuuliza ni lini Asisi angepelekwa kortini walitishwa na kufukuzwa kutoka pale. Mwandishi anaeleza haya: "...Hivi mnamweka humu mpaka lini? Juma

alimuuliza askari........Sasa unataka kutufunza kazi yetu au nini?..We have been at school askari alijibu "(uk 68)

Hizi zilikuwa ni mbinu zilizotumiwa na maafisa hawa ili waendelee kumnyanyasa Asisi pale kizuizini. Kifuja alishirikiana na mjukuu wake Huni kuendeleza biashara haramu ya ulanguzi wa madawa ya kulevya. Baada ya Huni kushikwa na polisi kwa tuhuma hizi Kifuja alitishia kuwafuta kazi askari hawa iwapo hawangetupilia mbali tuhuma hizo. Hatimaye Yusi mkuu alipatiwa bunda na kuambiwa anyamaze iwapo alipenda kazi yake. "Chai kidogo tu, chunga kazi isipotee.... Kifuja alisema baina ya kicheko na kuamuru... "(uk 108)

Vitisho ni mojawapo wa mbinu ambazo zimekuwa zikitumiwa na viongozi katika hali halisi ili kuendeleza uongozi wao dhalimu. Hali kama hii hujitokeza wakati wananchi wanaandamana na kudai haki zao. Askari hutumiwa kuwatisha wananchi kama hawa na wakati mwingine mauaji huwepo. Baadhi yao hujeruhiwa na hata kutiwa nguvuni. Pamekuwepo vilevile na visa vya viongozi kuwatisha walinda usalama wakiwa kazini wengine wakiwa na nia ya kutaka watambuliwe au hata wakiwa na jambo ambalo hawataki lijulikane.

### 4.2.5. Utepetevu katika utekelezaji wa sheria

Sheria zinapotungwa katika nchi fulani zinahitaji kufuatwa na kuheshimiwa na kila mwananchi ili kuhakikisha usawa katika jamii. Hata hivyo baadhi ya viongozi wanakosa kufuata sheria hizi na badala yake wanazikiuka bila adhabu yoyote. Mwandishi anatueleza kuwa mabasi yaliyokuwa yamemilikiwa na Kitambi yalikuwa yamekiuka sheria za magari ya uchukuzi nchini ikiwa ni pamoja na kutoangaliwa na maafisa wa trafiki....Ndiyo ya pekee yaliyoruhusiwa kubeba abiria katika barabara zilizopigwa marufuku magari ya uchukuzi kufika....Hali kama hii ya utepetevu katika utekelezaji wa sheria inayowawezesha wenye nguvu kukiuka sheria huhitilafiana na azma ya viongozi waadilifu ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Katika hali ya kawaida nchini, wabunge ndio wawakilishi wa wananchi katika Bunge la Taifa. Viongozi hawa wameshuhudiwa wakibatilisha baadhi ya sheria kwa manufaa yao wenyewe huku mwananchi wa kawaida akiendelea kutaabika kwa kukusa mtetezi licha ya kuwa yeye ndiye alichagua viongozi hawa.

#### 4.2.6 Matumizi Mabaya ya Mamlaka.

Viongozi wanapochaguliwa na wananchi wanatarajiwa kutumia mamlaka waliyonayo kuwatumikia wananchi wala si kuwakandamiza. Ni jukumu la viongozi kwa hivyo kuhakisha kila mwananchi analindwa na pia anatendewa haki. Hata hivyo katika nchi ya Kusinyika mambo ni tofauti na haya. Zinguo anatumia mamlaka yake vibaya anapomnyanyasa Sichana kimapenzi na hata kutishia kumfuta kazi nyumbani kwake. Anamnyamazisha Sichana ambaye alikuwa anapigania haki zake na hatimaye anaonekana akijigamba kuwa alijitakasa na msichana mdogo. Hii inakuwa changamoto kubwa kwa Sichana ambaye alikuwa anajaribu kuangazia dhuluma wanazopitia Wanakusinyika na hata wafanyakazi wenzake.

Zinguo anatumia mbinu hii vilevile kuwanyamazisha wananchi ambao wanaanza kulalamikia haki zao.Vijana wanapoungana na Wanakusinyika wengine Zinguo anatumia mamlaka kwa kuamuru Kaza mfuasi wake kuita askari ambao wanawapiga wananchi na hata kuwajeruhi. Anamwamrisha Kaza kama ifuatavyo:

**Zinguo** : .... kisu nimekinoa kikali
Mpinzani nitamtenganisha na mwili.
...apingaye atakula mkuki....(uk 60)

Maneno haya ya Zinguo yanaashiria kiongozi anayetumia mamlaka yake kwa njia ambayo haifai akiwa na nia ya kujinufaisha huku akilemaza juhudi za wananchi waliokuwa na azma ya kupigania ukombozi wao.

Viongozi katika mataifa mengi katika ulimwengu halisi wameshuhudiwa wakitumia ofisi za umma kwa njia zisizofaa. Badala ya kutekeleza wajibu wao kazini, wao huchukuwa nafasi waliyopewa ili kuwanyanyasa wananchi ili wao wanufaike. Visa vingi vya uhalifu nchini kama vya ufisadi na mauaji vimekuwa vikihusishwa na viongozi ambao wamekosa kuwajibika. Hili linakuwa ni pigo kubwa kwa wananchi ambao walichagua viongozi kama hawa.

#### 4.2.7 Dhuluma dhidi ya vijana

Vijana waliojaribu kupingana na uongozi wa Bwana Kifuja walikamatwa na kutiwa korokoroni kwa tuhuma zisizokuwa za ukweli. Asisi ni miongoni mwa vijana ambao walipigania haki za wanamabonde katika uongozi wa Kifuja. Baada ya kumaliza chuo

kikuu Asisi alijihusisha na masuala ya mabonde kiasi kwamba wengi walitamani awe mwenyekiti wa bodi ya usimamizi wa hazina ya ustawishaji wa eneo hilo. Kifuja alimpinga Asisi na kupendekeza Kipokeo awe mwenyekiti. Hii ilikuwa njia ya kumwadhibu Asisi ambaye alionekana kama mpinzani sugu wa uongozi wa Kifuja. Baada ya Kipokeo kukataa kumsaliti Asisi njama ilipangwa na Asisi akatiwa mbaroni kwa tuhuma za kumuua mhadhiri mmoja pale chuoni kama tunavyodokezewa na mwandishi kuwa: "Asisi alikumbuka ni Kifuja aliyemtuma mwanafunzi wa kike kumtoa uhai Profesa .....naye akasingiziwa" ( uk 90)

Asisi pia alikuwa mmoja wa waliopingana na kukubaliwa kwa magari ya Kifuja kubeba abiria katika jiji na huku mengine yakizuiwa. Hizi ni baadhi ya sababu zilizompelekea Asisi kushikwa. Katika kufanya hivi Kifuja aliweza kumnyima Asisi uhuru wake wa kuendelea kupigania haki za Wanamabonde na kwa hivyo, akapata fursa ya kuendeleza maovu yake.

Anao vilevile alitiwa mbaroni baada ya kupinga njama ya Kifuja, Mayowe na babake kuendeleza biashara ya mbao. Anao vilevile alilalamikia kutozwa kodi kwa Wanamabonde ambao hawakupata huduma kama vile za umeme na hata maji. Baada ya Asisi, Kipokeo na vijana wengine kwenda kumjulia hali Anao, nao pia waliwekwa mbaroni na kupelekwa mahakamani kwa kosa la kuvamia korti na hata kuhatarisha usalama wa wananchi. Hii ilikuwa ni mbinu ya kuwazuia vijana hawa kupigania haki zao na hata kushutumu uongozi mbaya wa akina Kifuja.

Kijasiri pia alitiwa kizuizini baada ya kuunda shirika la kupigania haki za kibinadamu ambalo lilimwezesha kushirikiana na wananchi wa mabandani ili kutetea haki zao. Humo ndimo Kijasiri aligundua kuwa Kifuja pamoja na Mayowe walikuwa wakiwatumia watoto wa shule kuuza madawa ya kulevya. Hatimaye Kijasiri alisingiziwa kuwa ndiye aliyekuwa akihusika na biashara hiyo haramu. Kama njia ya kumnyamazisha Kijasiri, mwanamke mmoja alipewa hongo na Kifuja ili atoe ushahidi wa uongo kortini kuhusu Kijasiri.

Uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahususi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Hali ya watetezi wa haki kushikwa na kuwekwa vizuizini si geni katika nchi yetu. Wanaondamana ili haki itendwe mara nyingi hujipata vizuizini madai

yakiwa eti walikuwa tisho kwa usalama. Mbinu hii hutumika ili kuwanyamazisha watu kama hawa ambao wanapigania haki zao. Wanaotiwa vizuizini mara nyingi huwa ni wanaoongoza maadamano miongoni mwa wananchi.

### 4.2.8 Ukosefu wa Haki Mahakamani

Mahakama vile vile ilitumiwa kuwakandamiza vijana ambao walikuwa wakipigania ukombozi wa Wanamabonde. Baada ya Asisi kwenda mahakamani kusikiliza yaliyokuwa yamemsibu Anao, jaji Kata alimkejeli Asisi kwa kumwambia: "Kijitu kuja kumtetea jitu? Uwaongoze hao watu wote, wewe peke yako kijitu ndani ya hawa majitu unatafuta nini" ( uk 85)Hatimaye mahakama ilisikiliza kesi za vijana hawa na kuamriwa wawekwe kizuizini wakati uchunguzi ulikuwa ukiendelea. Hii ilikuwa ni baada ya kesi ya Anao kuahirishwa bila sababu yoyote ya kuridhisha.Vijana hawa hawakupewa bondi hata baada ya kuomba jaji.

Kesi zilizopelekwa mahakamani na wanamabonde ili kupigania haki zao zililemazwa. Mfano mzuri ni kesi kuhusu kifo cha Halili mumewe Kijasiri. Kesi hii ilikuwa imekawia mahakamani kwa miaka ipatayo kumi na mitano. Kisasi chote hiki kilitokana na ukweli kuwa Kijasiri alikuwa miongoni mwa vijana waliokuwa wakipigania haki za Wanamabonde ambao walikuwa wamenyang'anywa mashamba yao.

Katika jamii yetu ukosefu wa haki mahakamani ni suala ambalo limekithiri sana. Baadhi ya wafungwa magerezani hudai kuwa hapakuwa na ushahidi wa kutosha uliotolewa mahakamani ili wawekwe gerezani. Malalamishi kama haya vilevile husikika miongoni mwa wananchi wanaongoja haki itendwe na mahakama. Baadhi ya kesi huchukua muda mrefu sana kabla ya kuamuliwa. Huu ni ukosefu wa haki kwa walalamishi ambao wanategemea mahakama kama hizi.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii utafiti wetu umebaini kuwa vijana wakiwa katika harakati za kuleta ukombozi, walikumbwa na changamoto anuwai ambazo zilinuia kulemaza juhudi zao za kufaulu. Changamoto hizi ziliwaathiri vijana hawa pamoja na waliokuwa wakishirikiana nao kupigana na viongozi dhalimu. Baadhi ya changamoto hizi ni

kama vile, vitisho, ukosefu wa haki mahakamani, kutiwa vizuizini na hata usaliti. Hata hivyo vijana walikabiliana na changamoto hizi bila ya kupoteza matumaini.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika utafiti wetu tulikuwa na malengo matatu ambayo ni: Kuchunguza aina za ukombozi zinazoletwa na vijana katika kazi teule, kuangazia vichochezi vya kupigania ukombozi katika kazi tulizoteua za Leonard Sanja na vilevile kubainisha changamoto zinazowakumba vijana katika kuleta ukombozi katika kazi husika. Tuliongozwa na nadharia ya uhalisia katika uchanganuzi wa data yetu. Utafiti wetu uliafikia malengo yetu na matokeo ni kama yafuatayo:

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Katika sura ya pili tulichunguza suala la ukombozi katika fasihi ya Kiswahili. Tulichunguza suala hili katika awamu tatu ambazo ni Afrika ya kale, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Tulieleza masuala mbali mbali katika awamu hizi ambayo yalikuwa vichochezi vya kupigania ukombozi. Baadhi ya masuala haya ni kama vile ukoloni, ukoloni mamboleo, ufisadi, na hata uongozi mbaya. Masuala haya ndiyo kiini hasa cha jamii zinazonyanyaswa kupata ari ya kupigania haki zao ili waweze kujikomboa.

Katika sura ya tatu tulibainisha aina mbalimbali za ukombozi katika kazi zilizoteuliwa za mwandishi Leonard Sanja.Kulingana na utafiti wetu ilibainika kwamba kulikuwepo na ukombozi wa aina mbali mbali katika kazi zile tatu. Aina hizi ni pamoja na ukombozi dhidi ya ukoloni mamboleo, ukombozi dhidi ya madawa ya kulevya, ukombozi wa kimawazo, ukombozi dhidi ya kunyanyaswa kwa mwanamke na ukombozi dhidi ya umasikini. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa palikuwepo na uwiano wa baadhi ya aina za ukombizi katika kazi tatu teule. Hivyo basi wahusika vijana wameshuhudiwa wakijitahidi kupigania aina hizi za ukombozi.

Sura ya nne ilishughulikia changamoto zilizowakumba vijana katika kupigania ukombozi. Changamoto zilizojitokeza zaidi ni zile ambazo zilikuwa mbinu za

viongozi dhalimu ambazo zilikusudia kulemaza juhudi za vijana katika kuleta mabadiliko. Vijana katika kazi hizi wanakabiliana na changamoto hizi bila kukata tamaa. Changamoto hizi ni kama vile usaliti wa vijana wenzao na hata wananchi, umasikini miongoni mwa wananchi ambao unawalazimu waendelee kuwachagua viongozi ambao wanawapa mavazi na vyakula wakati wa siasa, vitisho kutoka kwa viongozi dhalimu. Vitisho hivi vinanuia kuwatia hofu vijana ambao azma yao ni kuleta mabadiliko katika jamii zao ambazo zinanyanyaswa.Viongozi pia wanaonekana wakitumia mamlaka yao visivyo kwa nia ya kuwazuia vijana kuendelea kupigania haki zao. Wanatumia maafisa wa polisi kuwanyamazisha wananchi na hata kuwajeruhi.Mahakama ambayo inastahili kumpa mwananchi haki pia yanatumika kulemaza juhudi za vijana za kujikomboa. Haki haitendwi hata baada ya vijana kupeleka malalamishi yao. Licha ya changamoto ambazo vijana katika kazi hizi walikumbana nazo, utafiti wetu ulibainisha kuwa vijana hawa walijitahidi hadi wakazikomboa jamii zao kutoka uongozi dhalimu.

**5.3 Hitimisho**

Katika utafiti wetu tulihakiki nafasi ya vijana ya kuleta ukombozi katika *Yasinya, Zinguo la mzuka* na hadithi fupi ya “Mwavyaji wa Roho” katika *Diwani ya Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*.

Wahusika vijana wameangaziwa na waandishi mbali mbali katika kazi zao. Utafiti wetu ulijikita katika mwandishi mmoja wa kazi za fasihi ili kujaribu kubaini mwelekeo wake na jinsi anavyowakuza vijana katika kuleta ukombozi wa jamii zao. Utafiti huu umeonyesha mchango mkubwa wa vijana katika juhudi za kuleta aina mbali mbali za ukombozi kama inavyodhihirika katika kazi hizi. Vijana wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuzikomboa jamii zao kutokana na hali ngumu inazozikumba.

Utafiti huu umeonyesha kuwa licha ya kuwa vijana wamejitahidi kuzikomboa jamii zao wamekumbwa na changamoto anuwai za kulemaza jitihada zao. Changamoto hizi ni kama vile: upinzani mkali kutoka kwa viongozi, umasikini, usaliti kutoka kwa vijana wenzao, vitisho na matatizo mengine. Tumeonyesha vijana wakikabiliana na matatizo haya na hatimaye wameibuka washindi katika kuzikomboa jamii zao.

Kulingana na utafiti tulioufanya inaonekana kuna haja ya vijana kuungana ili kujinasua na hata kunasua jamii kutoka kwa matatizo yanayozikumba. Hili limejitokeza kwa uwazi katika *Yasinya.*

Ambapo wahusika wengi vijana wamejitahidi kupigana na viongozi dhalimu wanaolemaza maendeleo ya wanajamii.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti ulio na manufaa ni ule ambao mtafiti anaweza kutambua pengo linaloweza kuzibwa na watafiti wengine wa baadaye. Tunapendekeza ya kwamba wasomi wa baadaye watafiti kuhusu maswala mengine yanayohusiana na vyama katika kazi tofauti kifasihi.

# MAREJELEO


Acher, M.et al (1998). *Critical Realism: Essential Readings.* London.Routledge.

Arege, T. (2009). Mstahiki Meya: Nairobi. Vide- Muwa Publishers.

Donna,C.(2007). LiteraryRealism. Imepakuliwa kutoka http://www.scholastic.com/browse/article.jsp?id=3753924

Donna,C. (2007).Literary Realism. Imepakuliwa kutoka http://www.study.com/academy/lesson/the literary -realism-movement-a-response-to-romantism.html

Government of Kenya (*2010) Katiba ya Kenya.* Nairobi: Government Press.

Hegel, G. (1979*). Introduction to Aesthetics.* Oxford: Clarendon.

Hemming at el, (1978). *The Age of Realism*. Penguin Publishers, Middlesex, England.

Hope,R.(2004).Poverty in Africa. Imepakuliwa kutoka http://www.researchgate.net/publication/258175155. The Poverty Dilemma in Africa: Towards policies of including the poor.

Hussein, E.N (1971). Mashetani: Dar es salaam. Oxford University Press.

Kairu, M. W. (2005) .Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora Katika Fasihi Ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Karanja, P. N. (1990). Tamthilia Za Kiukombozi: Taswira ya Mwafrika katika Vita vya Ukombozi dhidi ya Ukoloni, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

*Kenya Bureau of statistics Census* (2009)

Kiango, S.D. (1992). Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Kenya. Katika *Baragumu*Juzuu ya 1 na 2 Kenya: Jarida la Kiswahili Chuo Kikuu cha Maseno.

Kihara, I. (2016). Nafasi ya vijana katika Riwaya Za Pendo La Karaha na Kovu Moyoni.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Kimani N. na Wafula, R.(2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*.Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kimani Njogu (1997).*Uhakiki wa Riwaya Za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Kimeu A. (2016). Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Kiongera K. J (2010). Mchango wa vijana katika mabadiliko chanya katika tamthilia nne za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Lomatoro. P. J (2014). Viwango vya Uhalisia na Ubunifu Katika *Cheche za Moto* na *Kaburi bila Msalaba.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Lugano , R.( 1989). Mwanamke Katika Riwaya Za Kezilahebi. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press.

Mbotela. J. (1934). *Uhuru wa Watumwa*. London: Sheldon Press.

Mbatia, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo yake*: Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation.

Mogambi, K (1983). Uhakiki wa Hali ya Wanyonge katika Riwaya tatu za S. Mohammed, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Msokile, M. (1993).*Misingi wa Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi: East African Educational Publishers.

Muriithi, F. (2016). Changamoto Zinazowakumba Vijana Katika riwaya ya *Upotevu*na *Dunia uwanja wa Fujo*.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mutua, J. (2007). Mitazamo ya Vijana Na Wazee Kuhusu Ukombozi Wa Mwanamke katika Tamthilia tatu za Kiswahili.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Mwazani E.(2015). Maudhui ya Ukombozi katika Diwani ya Jicho *la Ndani* . Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Naliaka, R.(2012). Uhakiki wa Hali ya Vijana Katika Riwaya ya *Vipanya Wa Maabara.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Ndanu, A. (2016). Maudhui ya Ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Ndegwa na Herbold. (1994). Africa to 2000 and Beyond: Imperative Political and Economic Agenda. Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999).*Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi:Jomo Kenyatta Publishers.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya Za Visiwani Zanzibar,* Nairobi: Nairobi University Press.

Nkonge, G. ( 2006). Athari za Udhanaishi katika *Kichwa Maji* na*Nguvu ya Sala* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Njoroge, A.W. (2014). Viongozi kama visababishi ya mabadiliko katika riwaya za Mwenda Mbatia.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Nyamwemba, R. (2012). Uchanganuzi Linganishi wa Maswala ya Vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na waandishi katika diwani ya *Tunu za Ushairi.* Tasnifu ya Uzamili, huo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Obure, E. (2012). Dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Sarara, M.M.( 1997) .Maudhui Katika Tamthilia za S.A Mohammed.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Sanja, L.  (2014).*Yasinya*. Nairobi: Focus Publishers.

Sanja,L.(mh) (2011).Diwani ya*Mwavyaji Wa Roho* na *Hadithi Zingine*.Nairobi: Focus Publishers.

Sanja,L. (2011).*Zinguo La Mzuka*.Nairobi: Focus Publishers.

Sayer, A. (1999). *Realism and social science London*: SAGE Publication.

Swingewood, A, (1975).*The Novel and Revolution*. London. Macmillan Press limited

Wa Thiong'o, N. (1986).*Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature*: Heinemann Educational Books.

______. (1981).Writers in Politics: London: Heinemann Educational Books.

Walibora, K. (2012). Kidagaa Kimemwozea: Nairobi:Target Publishers Limited.

Wamitila,K.(2002).*Uhakiki wa Fasihi*:*Misingi na Vipengele Vyake*.Nairobi.Phoenix Publishers.

Wafula, R. (1999). Uhakiki wa tamthilia tatu kuhusu vijana.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Wafula, R. M. na Njogu, K.(2007).*Nadharia Za Uhakiki Wa Fasihi*.Nairobi: The Jomo KenyattaFoundation.

Wellek, R.( 1960) .“The concept of Realisim literary scholarship”*Neophilologus XI*

Were, G.S (1983). *Leadership and undevelopment in Africa*. Nairobi: Gideon S. Were Publishers.